SportPesa
TZS. 1,171,243,460
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Watatu** kortini baada ya miaka 20 kwa tuhuma za mauaji

UKURASA 3




Nipashe
Jumanne Aprili 19, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580920
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ
0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# Filamu ya Royal Tour kuifungua Tanzania duniani

• **Watalii** kutoka Marekani kumiminika, kuzinduliwa maeneo mengine... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akiandaa filamu ya Royal Tour katika mbuga ya wanyama ya Serengeti. Filamu hiyo imezinduliwa jana nchini Marekani. **PICHA: MAKTABA**

## Mamba waua watu sita Mto Ruvu

UKURASA 3



## Madini yachimbwa katika hifadhi ya taifa

• **Kampuni** yapewa leseni kinyume cha sheria...*Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **SIMBA: NGUMU KWA ORLANDO SAUZI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Ofisa Mawasiliano wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Elizabeth Eusebius akizungumza na wakazi wa kata ya Mbwawa Mlandizi Mkoa wa Pwani, katika mkutano uliolenga kuhamasisha wananchi kupatiwa huduma ya majisafi baada ya kutekelezwa kwa mradi wa maji Mbwawa uliogharimu kiasi cha Sh. Bilioni 1.1. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Filamu ya Royal Tour kuifungua Tanzania

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema kuwa filamu ya Royal Tour iliyozinduliwa jana na Rais Samia Suluhu Hassan, jijini New York, Marekani, itaitangaza Tanzania duniani, huku ikileta maelfu ya watalii kutoka nchini humo.

Katika uzinduzi huo uliofanyika katika jumba la Makumbusbo la Guggenheim 89th Avenue jijini New York, ulihudhuriwa na wadau wa utalii na watu mashuhuri wapatao 300, huku ikipambwa na burudani mbalimbali.

Filamu hiyo iliyochukua takribani saa moja imesheheni vivutio mbalimbali vya utalii, sanaa na burudani vinavyopatikana nchini Tanzania, vilivyotambulishwa kwa kuelezewa kwa kina na Rais Samia.

**MUKTADHA WA FILAMU**

Akizungumzia filamu hiyo wakati wa mjadala wa viongozi wa serikali na taasisi zake uliofanyika kwa njia ya mtandao wa Zoom, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, kipindi cha filamu ya saa moja inayotangaza utalii wa Tanzania kiliratibiwa na mtangazaji mashuhuri nchini Marekani, Peter Greenberg .

Alisema mwandishi huyo hushawishi viongozi wa nchi kuwa mbele kutangaza vivutio vya nchi yao na Tanzania ni nchi ya tisa duniani kushiriki mradi huo unaolenga kuitangaza nchi kwenye utalii ili ijulikane duniani.

"Kwa ujumla ni kui 'repackage' (kuviweka pamoja) nchi yetu ili ijulikane kote duniani, iwe ni sehemu ambayo watu wawe wanakuja siyo tu kutembea, kuona wanyamapori lakini pia kurekodi matukio makubwa ya kuburudisha," alifafanua.

Dk. Abbas ambaye ni Mwenyekiti wa kamati ya Royal Tanzania Tour, alisema ni mradi wa kwanza wenye kuhakikisha mazuri ya Tanzania yanafahamika ulimwenguni ikiwamo utalii, viwanda, sanaa na utamaduni.

Aliongeza kuwa filamu hiyo imezinduliwa Marekani kwa sababu lengo ni kuitangaza nchi kimataifa na kwa kuanzia wamealikwa watu washuhuri ikiwamo wafanyabiashara, wadau wa utalii na burudani.

**UMUHIMU WA ROYAL TOUR**

Naye, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, alisema uzinduzi wa filamu hiyo unakwenda kufungua milango ya uwekezaji katika utalii pamoja na sekta nyingine, jambo litakaloongeza kipato cha mtu mmoja na taifa.

"Sisi Wizara ya Maliasili na Utalii, tunamshukuru sana Rais kwa maana hili ni jukumu letu sote la msingi. Tukisema Royal Tour inakwenda 'ku-ibrand'(kuitangaza) Tanzania watu hawatuelewi. Tanzania tuna vivutio vingi sana vya utalii ingawa siyo wote wanavijua na utalii unachangia katika pato la taifa kwa asilimia 17," alisema.

Alisema filamu hiyo inakwenda kutangaza utajiri wa utaliii uliopo Tanzania ikiwamo Hifadhi za Taifa 22, mapori ya akiba 27, mapori tengefu 42, kilomita 1,428 za fukwe ya Bahari ya Hindi, Mlima Kilimanjaro na Hifadhi za Wanyamapori za Jamii (Wildlife Management Area) 33.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Said, alisema Royal Tour inakwenda kufungua milango ya watalii Zanzibar kwa kuwa wageni wanaokuja bara watavutiwa kwenda Zanzibar pia.

"Wamarekani wao wanapenda kutumia pesa, 'they tip well' (bakshishi safi) wanapenda huduma nzuri na wanafurahia wanachokiona, sisi lazima tuitumie fursa hiyo. Lakini huduma zetu lazima tuziweke katika mfumo ambao utawaridhisha,"alibainisha.

Aidha, alisema kuwa biashara ya utalii siyo ya serikali pekee, hivyo aliziomba sekta binafsi kushirikiana na serikali katika kukuza utalii.

Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), Dk. Maduhu Kazi, alisema anajivunia kuwa sehemu ya mpango huo kwa kuwa wanategemea kujitokeza fursa nyingi za uwekezaji kupitia filamu hiyo.

"Kwa upande wa uwekezaji tumejiandaa vizuri sana na tunaona kuwa kutakuwa na fursa nyingi, ndani ya siku mbili kutakuwa na (Makubaliano Maalum (MOU's) kadhaa ambazo zitasainiwa baina ya kampuni za nyumbani na za huku Marekani. Bado tunaendelea kuziaccount...kwa zile ambazo zimekashakamilika tunaona kuwa kuna uwekezaji mkubwa ambao unakuja nchini mwetu," alisema Dk. Maduhu.

Aliongeza kuwa aina ya wawekezaji ambao Rais Samia atakwenda kukutana nao ni wale wa hali ya juu hali inayoleta matumaini ya uhakika wa kupata wawekezaji.

Alisema licha ya kuvutia wawekezaji wa Utalii wamejipanga pia kuwavutia wawekezaji katika kilimo 'agroprecessing' (usindikaji mazao) kwenye maeneo ambayo nchi inahitaji zaidi wawekezaji ikiwamo mafuta ya kula ambalo linaigharimu nchi Sh. bilioni moja kwa mwaka.

**TTB KAZI NDO IMEANZA**

Mkurugenzi wa Masoko katika Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Felix Michael, alisema ikiwa kama wahusika wakuu wa kutangaza vivutio vya utalii filamu ya Royal Tour wanaichukulia kama ni kifaa cha kimkakati cha kuitangaza biashara ya utalii kimataifa.

"Na hii filamu kwetu tunaichukulia kama 'promotion tool' ya kimkakati, ambayo inakwenda kujibu maswali magumu, kama upotoshaji ambao umekuwapo. Kuna baadhi ya watu duniani bado wanaamini kuwa Mlima Kilimanjaro upo nchi jirani. Kuna watu wanaamini kuwa Hifadhi ya Taifa Serengeti (SENAPA) ipo nchi tofauti na nchi yetu," alifafanua.

Alisema wanatarajia kupitia filamu hiyo kutumia mabalozi wao wa hiyari, kutangaza na kuhamasisha utalii katika nchi za kimakakati Marekani ikiwamo, lakini pia kupanga mikakati mingine ya kuitangaza nchi.

Rais Samia aliondoka nchini Aprili 14, mwaka huu kuelekea nchini humo kwa ziara ya kikazi, ambayo pamoja na mambo mengine, anatarajia kuzindua kipindi maalum cha kutangaza utalii wa nchi yake katika majiji ya New York na Los Angeles nchini humo.

Pia, atazungumza na watanzania wanaoishi nchini humo kueleza mipango mbalimbali ya serikali, na kuwahimiza kuunga mkono juhudi za kuendeleza nchi.

# Madini yachimbwa katika hifadhi ya taifa

## ●Kampuni yapewa leseni kinyume cha sheria

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini uendeshaji wa shughuli za uchimbaji madini ndani ya Hifadhi ya Taifa Saadani kinyume cha sheria.

CAG Charles Kichere anabainisha hayo kwenye ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Jumanne ya wiki iliyopita.

Anasema alibaini kuwa Kampuni ya M/S Seasalt yenye leseni Na.ML 05/92 ya uchimbaji wa madini ambayo inatoa haki kwa kampuni hiyo kufanya shughuli za uchimbaji wa madini ya chumvi ndani ya eneo la Hifadhi ya Saadani lenye ukubwa wa ekari 2,400 linalomilikiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 281 la mwaka 2005.

"Ukaguzi wangu ulibaini kuwa ekari 728.17 kati ya 2,400 ilizopewa kampuni hiyo, tayari zilikuwa zimeendelezwa bila kibali cha TANAPA, jambo ambalo ni kinyume cha Kifungu cha 95(1) (c) cha Sheria ya Madini, Sura ya 123 inayomtaka mwenye leseni ya kuchimba madini kutotumia haki ya leseni kuendeleza ardhi ambayo ni mali ya TANAPA iliyotangazwa chini ya Sheria ya Hifadhi za Taifa, isipokuwa kwa idhini ya mwenye mamlaka ya udhibiti wa hifadhi nchini Tanzania," anafafanua.

**MBWA, KUKU HIFADHINI**

CAG pia anasema alibaini kuwa wafanyakazi wa kampuni hiyo walikuwa wakifanya shughuli za kibinadamu ndani ya hifadhi kama vile kufuga wanyama kama mbwa, kuku na mbuzi.

Ana angalizo kwamba vitendo hivyo vinahatarisha ustawi wa wanyamapori kwa kuwa kuna uwezekano wa kusambaza magonjwa kutoka kwa mifugo kwenda kwa wanyamapori.

"Vilevile, shughuli za uchimbaji wa madini husababisha uchafuzi wa mazingira utokanao na kumwagika kwa mafuta yanayotumika kwenye mitambo, takaoevu, uchomaji wa taka ngumu na kelele ndani ya hifadhi.

"Kwa maoni yangu, shughuli hizi zinahatarisha mfumo wa ikolojia wa hifadhi na hivyo kusababisha kutokuwapo kwa uhakika wa uendelevu wa Hifadhi ya Taifa Saadani.

"Ninapendekeza TANAPA ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na mamlaka zingine za serikali ili kutathmini athari za uchimbaji wa madini katika mfumo wa ikolojia wa Hifadhi ya Taifa Saadani na kuchukua hatua stahiki," CAG anatoa hoja.

**KIWANDA HIFADHINI**

CAG pia anasema amebaini Kiwanda cha Sukari cha Bagamoyo chenye namba ya usajali 3565-1 kilipewa na serikali ardhi ya hekta 10,000 ndani ya Hifadhi ya Taifa Saadani yenye hatimiliki Na. 156361MG iliyotolewa Oktoba Mosi, 2016 ikiwa na hatimiliki ya kipindi cha miaka 66.

Anafafanua kuwa mapitio yake yalibaini kuwa maeneo matano muhimu ya uhifadhi kati ya manane yalikuwa ndani ya hekta 3,441 ambazo ni kati ya hekta zilizotengwa kwa ajili ya mashamba ya miwa.

CAG Kichere anasema maeneo hayo ambayo yako ndani ya eneo la umiliki wa shamba la miwa, yana athari kubwa kwa uhifadhi kwa vile ndiyo maeneo yanayotumiwa na wanyamapori kuzaliana, njia za kupita wanyamapori (shoroba), vyanzo vya maji vya Mto Wami na ni mlango wa maji wanayokunywa wanyamapori.

Vilevile, CAG anasema eneo hilo ni la msitu wa mikoko inayotumika katika udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na ni mazalia ya kasa wa kijani.

"Zaidi, ukaguzi wangu ulibaini kuwa eneo lililotolewa kuwa shamba la Sukari la Bagamoyo ndilo eneo linalotegemewa wakati wa kiangazi kutokana na asili yake ya kijani kibichi na malisho ya mimea.

"Licha ya serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutembelea hifadhi hiyo na kuelekeza umbali wa mita 200 kati ya 500 kutoka ukingo wa Mto Wami ubaki kwenye eneo la hifadhi hiyo ikiwa pamoja na mita 60 na 200 kutoka ukingo wa mto huo kama eneo la ulinzi, hadi wakati wa ukaguzi huu, maelekezo ya wizara hizo yalikuwa hayajatekelezwa.

"Kwa maoni yangu, shughuli za kiwanda zinaweza kuathiri mfumo wa ikolojia na kuhatarisha maisha ya wanyamapori na wakati huo huo, maji yenye kemikali za kilimo yanaweza kuathiri wanyamapori na samaki wa ukanda huo wa Bahari ya Hindi.

"Ninapendekeza serikali na Bodi ya Wadhamini ya TANAPA kutathmini kwa kina athari za uendeshaji wa mashamba ya miwa ndani ya Hifadhi ya Taifa Saadani na kutafuta njia bora ya kukabiliana na hali hiyo, na matokeo ya tathmini hiyo yawe ni marejeo kwa matumizi ya baadaye," CAG anatoa hoja.

# Mamba waua watu sita Mto Ruvu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAMBA wamelalamikiwa kuwa tishio kwa wakazi wanaozungukwa na Mto Ruvu wilayani Kibaha, mkoani Pwani, huku watu sita wakidaiwa kuliwa.

Wanadai kuwa wamekuwa wakikumbwa na kadhia hiyo wakati wa kusaka maji kwenye mto huo.

Malalamiko hayo yanatokana na watu sita kuuawa na mnyama huyo katika Kitongoji cha Kigogo, Kijiji cha Kimaramisale Kata ya Dutumi Halmashauri ya wilaya ya Kibaha kwa kuliwa na mnyama huyo kwa nyakati tofauti wakichota maji kwenye Mto Ruvu.

Malalamiko hayo yalitolewa na wakazi kadhaa akiwamo Said Kikwembe wakati wa mkutano wa Mbunge wa Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo, alipokuwa akizungumza na wananchi kuhusiana na kero mbalimbali na kujadiliana namna ya kuzitatua.

Kikwembe alisema watu hao wameliwa na mamba kwa nyakati tofauti wakiwa wanasaka maji kutokana na kijiji chao kutokuwa na maji ya bomba.

Naye Hamisi Maisha na Ashura Mkwayu wameiomba Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kuangalia uwezekano wa kuwavuna mamba hao ili kuondoa adha inayowakumba wananchi hao ambao ni lazima wafike kwenye mto huo kupata huduma ya maji.

Ashura alisema kwa sasa hawana amani kutokana na mamba kushamiri katika eneo hilo ambalo kwao ni tegemeo la kupatia maji kwa matumizi ya nyumbani.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Salum Bong'o, alisema kuwa katika mkasa huo wa mamba alipoteza baba yake mzazi aliyeliwa na mamba miezi michache iliyopita.

Alimuomba Mbunge Mwakamo kusimamia mradi wa maji katika kijiji cha Kimara Misale ili uwafikie Kigogo waondokane na adha ya kuchota maji katika Mto Ruvu kuepukana na tishio la mamba.

"Maji hapa Kigogo ni tatizo kubwa ndio linalosababisha vifo vya ndugu zetu, tunakuomba Mbunge huo mradi wa maji unaoendelea makao makuu ya Kijiji chetu Kimara Misale uharakishwe utufikie na huku kwetu," alisema mwenyekiti huyo.

Akizungumza na wakazi hao Mbunge Mwakamo aliwapa pole kwa matukio hayo ambapo alieleza kuwa mradi wa Kimara Misale unaendelea kutekelezwa kwa kasi na ukikamilika utamaliza kero ya tishio la mamba.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470DODOMA,
21.03.2022

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya **tarehe 19.04.2022 hadi 05.05.2022** kampuni ya Spedag Interfreight itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Holili kuelekea Moshi, gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW052Z / ZG3212**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   **Urefu - Mita 28.4 Upana - Mita 5.0 Kimo - Mita 5.6**
3. Njia itakayotumika: Holili hadi Moshi kupitia Soweto, gari litasafiri muda wa mchana tu ( **Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

## Samia: Vijana changamkieni TEHAMA

**Na Benny Mwaipaja,** NewYork

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka watanzania hususan vijana, kuchangamkia fursa za maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Rais ametoa wito huo Mjini New-York nchini Marekani, katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alipozindua Mtandao wa NALA (NALA APP) utakaotumiwa na watanzania waishio Marekani kutuma fedha nchini Tanzania kidijitali.

Alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya NALA, Raia wa Tanzania, Benjamin Fernandes na Timu yake, kwa kubuni Application hiyo ambayo itarahisisha utumaji wa fedha kutoka nchini humo kwenda Tanzania hatua ambayo itasisimua uchumi wa nchi na kuharakisha maendeleo ya wananchi watakaofaidika na huduma hiyo.

"Benjamin Fernandes na Timu yako ni miongoni mwa vijana wabunifu waliojikita katika masuala ya teknolojia ambao Serikali inawaunga mkono hususan wakati huu ambapo nchi inajenga uchumi wa kidijitali ambao matokeo yake yanatarajwa kuwa ni kukuza ajira, kuchangia pato la Taifa na kukabiliana na changamoto zote za kiuchumi na kijamii," alisema Dk. Nchemba.

Alisema kuwa Serikali imewekeza fedha nyingi kwenye miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kujenga mkongo wa Taifa uliounganishwa na nchi nyingine za kiafrika zikiwemo Burundi, Rwanda, Kenya, Malawi, Uganda na Zambia na hivi karibuni nchi za DRC na Msumbiji zitaunganishwa.

Fernandes alisema Application iliyozinduliwa nchini Marekani, inafanyakazi katika nchini nyingine 9 duniani na aliibuni kwa ajili ya kusaidia utumaji wa fedha kwa nchi za Afrika.

## Watatu mahakamani baada ya miaka 20 kwa madai ya kuua

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WATU watatu wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma za mauaji ya kuua mwanamke mkoani Mtwara miaka 20 iliyopita.

Watuhumiwa hao ni wakazi wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Masasi kwa tuhuma za mauaji ya mwanamke aliyetambulika kwa majina ya Nora Hamisi.

Nora mkazi wa Kata ya Mkuti wilayani Masasi, aliuawa na mwili wake kutupwa katika Mtaa wa Machinjioni katika Kata ya Mkuti.

Watuhumiwa hao walifikishwa kortini mwishoni mwa wiki mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Masasi, Batista Kashusha na kusomewa mashtaka ya mauaji wanayodaiwa kuyafanya miaka 20 iliyopita.

Mwendesha Mashtaka wa Polisi Insepta Jovina alidai kuwa watuhumiwa hao wanakabiliwa na kesi hiyo namba 2 ya mwaka 2002 mbele ya Mahakama hiyo.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Rajabu Songo (34), mkazi wa mtaa wa Machinjioni Kata ya Mkuti wilayani Masasi, Stanley Mtweve (32), mkazi wa Mtaa wa Makaburini Kata ya Mkuti wilayani Masasi na Yusuph Pahala (30), mkazi wa Mtaa wa Maendeleo Kata ya Mkomaindo wilayani Masasi.

Inspekta Jovina alidai kuwa watuhumiwa hao walimuua Nora kisha kuuchukua mwili wake na kuutupa katika Mtaa wa Machinjioni kisha kutoweka.

Alidai waliutupa mwili eneo hilo kwa lengo la kupoteza ushahidi, lakini baada ya uchunguzi wa Jeshi la Polisi walikamatwa.

Watuhumiwa hawakutakiwa kuzungumza lolote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji.

Kwa mujibu wa sheria, mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji ni Mahakama Kuu.

Wote walirejeshwa mahabusu na kesi hiyo itatajwa tena Aprili 24, mwaka huu.

**CONTRACTORS REGISTRATION BOARD**

**REGISTRATION STATUS UPDATE**

The Board would like to inform all contractors registered in **CLASS FIVE** as of 30.06.2017 that Pursuant to section 4(q) of the Contractor Registration Act No. 17 of 1997, it is now updating contractors' information in the database to match with the current status of the contractor in terms of shareholding status, official addresses, staffing level and equipment holding capacity.

In order for the said information to be effectively and timely updated, the said contractors are hereby instructed to submit the duly filled **REVIEW INFORMATION FORM (already posted in your postal addresses and can also be downloaded on the website www.crb.go.tz**).

In addition, the following information should be submitted along with the said form:

1. Current Business Registration and Licensing Authority (BRELA) Search Report.
2. Covering letter indicating inter alia, which names among the shareholders shown in the Brela search, stands as Managing and Technical Director in the construction company.
3. Resolution of the Board of Directors and Affidavit as a commitment that the submitted information is correct and can be used to update your company status in the data base.

The said information should reach the Board latest by 30th April 2022.

**REGISTRAR**

216795702

# CAG abaini tatizo mapato ya TANAPA kukusanywa TRA

Na Sanula Athanas, DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini kuwapo upungufu wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika hifadhi za taifa uliochangiwa na uamuzi wa serikali kuagiza mapato ya sekta hiyo yakusanywe na Mamlaka ya Mapato (TRA).

Kabla ya mwaka 2020/21, mapato ya utalii yalikuwa yanakusanywa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), lakini kuanzia Julai Mosi, 2020, serikali iliagiza mapato hayo yakusanywe na TRA huku serikali ikiahidi kutoa fedha zinazohitajika kwa hifadhi hizo kulingana na bajeti za hifadhi.

Hata hivyo, katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumanne iliyopita, CAG Charles Kichere anasema amebaini tofauti kubwa kati ya bajeti zilizoidhinishwa kwa ajili ya hifadhi hizo na kiasi kilichotolewa na serikali kugharamia miradi ya maendeleo ya hifadhi husika.

"Kwa mfano, NCAA ilitarajia kupokea Sh. bilioni 31.21 kulingana na bajeti yake ya shughuli za maendeleo, lakini serikali ilitoa Sh. bilioni 10.27 tu, sawa na asilimia 33 ya bajeti iliyoidhinishwa. Hivyo, miradi iliyotekelezwa ilikuwa 15 tu kati ya 36.

"Pia nilibaini kuwa kiasi hicho (Sh. bilioni 10.27) kilichelewa kutolewa kwa muda wa miezi saba, ambapo mamlaka iliomba fedha hizo tarehe 21 Oktoba 2020 lakini serikali ilizitoa tarehe 5 Mei 2021.

"Kadhalika, nilibaini kuwa bajeti ya maendeleo ya TANAPA ilikuwa Sh. bilioni 69.52 lakini ni Sh. bilioni 26.51 tu, sawa na asilimia 38 ndiyo ziliidhinishwa kutolewa," anabainisha.

CAG ana angalizo katika hilo, akisema kuwa kutolewa kwa fedha chini ya bajeti kulichangia kutotekelezwa kwa shughuli za maendeleo ya hifadhi zinazohusiana na miundombinu, uhifadhi na huduma za utalii.

"Kwa maoni yangu, mwenendo huu ukiendelea, utaleta athari mbaya kwa utalii kutokana na uchakavu wa miundombinu na ukosefu wa vifaa vinavyosaidia kuboresha huduma za kitalii. "Hivyo, ninapendekeza serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo za kutosha na kwa muda unaostahili ili mamlaka za hifadhi ziendelee kutoa huduma bora kwa watalii na kuvutia watalii wengi ili kuongeza pato litokanalo na Sekta ya Utalii," CAG anawasilisha hoja yake.



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Injinia Felchesmi Mramba (katikati), akikagua eneo lenye nishati ya jotoardhi Kijiji cha Nanyala, wilayani Mbozi, mkoani Songwe. Kulia ni Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), Mhandisi Mathew Mwangomba na (kushoto) ni Mhandisi Shakiru Idrissa, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara TGDC. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kada CCM adaiwa kuuawa kwenye ugomvi wa kisiasa

Na Samson Chacha, TARIME

Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi CCM Tawi la Sokoni Kata ya Sirari wilayani Tarime mkoani Mara, Moshi Sayi Maduhu, ameuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali kifuani karibu na shingoni baada ya kutokea ubishi wa kisiasa kati yake na mfuasi wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Senga Shuri. Kufuatia hali hiyo, Shauri ambaye ni fundi baiskeli anashikiliwa na Jeshi la Polisi kituo cha Sirari.

Kamanda wa Polisi Tarime Rorya ACP William Mkonda, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema lilitokea Jumamosi 16 jioni katika Kitongoji cha Sokoni wakati wa ugomvi kati ya Maduhu na Shuri aliyekuwa na kisu kisha kumchoma kifuani na kumsababia kifo. Alisema mtuhumiwa amekamatwa na wanamhoji na baadae atafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Kamanda Mkonda alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi katika wilaya za Tarime na Rorya kuacha kutembea na silaha, na kwamba halitasita kuwachukulia hatua kali watu wote wanaokamatwa wakitembea na silaha na kujichukulia sheria mkononi badala yake kama kuna malalamiko watu waende kwenye vyombo husika ili haki iweze kupatikana.

Wakizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki Diwani wa Sirari kupitia CCM, Amos Sagara , Diwani wa Regicheri, John Bosko, Diwani wa Gwtiryo, Nashon Mchuma, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Sokoni kupitia CCM, Bob Benjamin, mjumbe wa mkutano mkuu CCM Wilaya ya Tarime, Laurent Nyablangeti ,

Katibu Kata CCM Kata ya Gwitiryo Hidaya Peter, Mwenyekiti wa Kijii cha Gwitiryo, Joseph Timuti na wanachama wa CCM kata hizo, walisema kuwa CCM Sirari na kata jirani za Gwitiryo na Regicheri wamepata pigo kubwa kutokana na kifo cha Maduhu.

Walisema kuwa Maduhu alikuwa kiongozi asiyependa kushindwa kwa jambo alilokuwa analitetea, na kwamba amepigania chama chake hadi umauti unamkuta alinadi sera na ilani katika kata zote tatu bila kuchoka, na ameacha alama ya kujitolea.

# Waagizaji magari waomba serikali kupunguza ushuru

Na Romana Mallya

SIKU chache baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kutamka kuwa magari yaliyotengenezwa chini ya mwaka 2010 yasiingizwe nchini, waagizaji na wauzaji wa magari wameomba serikali ipunguze ushuru ili Watanzania waweze kuyaagiza matoleo mapya.

Aprili 10 mwaka huu, Majaliwa alifanya ziara ya kushtukiza katika Bandari ya Dar es Salaam na kusema Tanzania haitakiwi kuwa dampo kwa kuleta magari yaliyopitwa na wakati.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, waagizaji na wauzaji wa magari wamesema wateja wao wamekuwa wakiagiza matoleo ya zamani kwa sababu ya bei zake kuwa chini ikilinganishwa na matoleo mapya.

Issa Kinga kutoka Kampuni ya Jan International Limited inayojishughulisha na uuzaji magari, alisema asilimia kubwa ya wateja hununua magari ya mwaka 2005, 2006 na 2008 kutokana na bei yake kuwa chini.

Alitolea mfano kwa wanunuzi wa magari madogo yaliyotengenezwa mwaka 2010 kushuka chini bei zake huwa ndogo ambazo huanzia Sh. milioni 15 kulingana na aina ya gari.

"Alichokisema Waziri Mkuu ni jambo zuri na litatusaidia kuendelea kuwa na magari ya matoleo la kisasa, ila kama wanataka kufanya hivyo washushe ushuru kwa sababu kila Mtanzania ana uwezo wa kununua gari tatizo kubwa huwa ni ushuru mkubwa kuliko bei ya uagizaji gari," alisema.

Meneja wa SBT Japan ofisi ya Tanzania, Hassan Iddi, alisema mteja anapokwenda kwao na kuchagua gari la toleo la zamani siyo kwamba analipenda zaidi bali ni kutokana na thamani yake sokoni.

"Mfano mtu anataka kuagiza RAV4 ya mwaka 2012 thamani ya kununua gari hilo Japan ni kubwa na ushuru kwa makisio mteja anatakiwa awe na fedha siyo chini ya milioni 40.

"Wakati RAV 4 toleo la zamani mfano ya 2004 unaweza kutumia Sh. milioni 25 wakati toleo la sasa kuagiza peke yake unaweza kutumia siyo chini ya milioni 20."

Iddi alisema wateja wengi wa Tanzania kutokana na biashara zilivyo kipato chao hakikidhi magari ya toleo la sasa.

"Siyo kwa watumishi wala wafanyabiashara kwenye asilimia 100 labda wanaoagiza magari ya toleo la sasa ni asilimia tano. Endapo itakuwa hivyo kama walivyoelekeza kwa sababu bado kauli yake haijatolewa ufafanuzi kama yazuiwe kabisa ya chini ya mwaka 2010 au ni mkakati upi utawekwa.

"Labda ya zamani wataongeza kodi kidogo au kuzuia kabisa, wakizuia kabisa maana yake ni kwamba biashara lazima ishuke s ana kwa sababu ni kundi dogo la wanaoagiza magari ya sasa."

Idd alisema wanasubiri ufafanuzi wa kauli hiyo ili kuelimisha wateja wao kwa sababu tangu itoke wateja walioagiza magari ya chini ya mwaka 2010 wamekuwa wakipiga simu kwao kuulizia hilo.

Kuhusu ushauri wao kwa serikali, Idd alisema wataheshimu maagizo yote yatakayotolewa, ingawa waagizaji wanaona Watanzania wengi kipato chao kinamudu kununua magari ya zamani.

"Sera ingetakiwa iangalie kwa namna gani magari yatakaguliwa hata kama ni ya zamani, kwa sababu hii imeenda sambamba na kubadilisha ukaguzi wa magari kutoka Tanzania na kurudi nje ya nchi, waweke vigezo ya kuangalia ubora wa gari hata kama litaagizwa la 2004 basi liwe katika hali nzuri," aliomba.

Katika ziara hiyo, Majaliwa alisema Bunge limeshapitisha sheria kuwa magari yote yanayoingizwa nchini yawe yametengenezwa baada ya mwaka 2010 kuja huku mbele.

"Tunaangalia viwango, ni viwango gani wakati sisi siyo watengenezaji, TBS imeeleza maeneo ambayo wanayahakiki magari yetu mengi yanayoingia nchini ni pamoja na yale yanayoagizwa na Watanzania, kama ni kutumika yanakuwa yametumika mwaka mmoja au miwili.

"Sasa yanapokuja hapa lazima tujiridhishe hatuleti magari yaliyopitwa na wakati na Tanzania ikawa dampo, wajibu wa TBS ni kufuatilia gari limetengenezwa lini, je, tairi zilizoingia ni nzima gari lina hali gani, magari mengine mmeyaona ni makukuu."

TANGAZO

# NATIONAL INSURANCE CORPORATION OF TANZANIA LIMITED (NIC)

# STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2021

SISI NDIYO BIMA

## STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2021

| | Notes | General insurance 30 June 2021 | Life assurance 30 June 2021 | Total 30 June 2021 | Total 30 June 2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 |
| Property and equipment | 4 | 1,815,020 | 8,412,213 | 10,227,233 | 12,194,904 |
| Investment properties | 5 | 34,085,047 | 79,823,120 | 113,908,167 | 93,105,169 |
| Right of Use Asset | 6 | 119,708 | - | 119,708 | - |
| Inventories | 7 | 231,339 | 103,313 | 334,652 | - |
| Intangible asset | 8 | 57,575 | 40,043 | 97,618 | 80,293 |
| Work in Progress (Computer Software) | 9 | 533,084 | - | 533,084 | 328,720 |
| Deferred acquisition costs | 10 | 506,348 | - | 506,348 | 460,123 |
| Investment securities | 11 | 2,694,252 | 30,446,827 | 33,141,079 | 30,226,226 |
| Investment in Ubungo Plaza Ltd | 12 | - | 21,081,456 | 21,081,456 | 21,004,148 |
| Re-insurers share of insurance contract provisions | 13 | 16,794,260 | - | 16,794,260 | 11,915,982 |
| Insurance and other receivables | 14 | 36,197,513 | 22,364,364 | 58,561,877 | 84,639,011 |
| Treasury Bonds | 15 | 81,445,744 | 26,654,388 | 108,100,132 | 50,070,500 |
| Treasury Bills | 16 | 866,850 | 932,700 | 1,799,550 | 1,513,025 |
| Fixed deposits with banks | 17 | 8,046,264 | 2,338,214 | 10,384,478 | 19,525,106 |
| Cash and cash equivalents | 18 | 19,851,891 | (3,950,222) | 15,901,669 | 25,293,454 |
| **Total assets** | | **203,244,895** | **188,246,416** | **391,491,311** | **350,356,661** |
| **LIABILITIES** | | | | | |
| Deferred tax liability | 19 | 5,148,202 | 6,529,656 | 11,677,858 | 9,530,827 |
| Insurance contract provisions | 20A | 23,056,667 | 28,320,950 | 51,377,617 | 45,715,307 |
| Unearned Premium Reserve | 20B | 16,999,103 | - | 16,999,103 | 23,880,253 |
| Policyholders' Fund | 20C | - | 107,375,980 | 107,375,980 | 99,582,068 |
| Payables to re-insurers | 21 | 27,319,199 | - | 27,319,199 | 23,595,345 |
| Pen save deposits | 22 | - | 164,498 | 164,498 | 156,200 |
| Other payables | 23 | 40,528,538 | 6,699,176 | 47,227,714 | 63,506,519 |
| Gratuity payable | 23 | - | - | - | 329,235 |
| Income tax payable | 39B | 12,801,432 | - | 12,801,432 | 11,897,606 |
| **Total liabilities** | | **125,853,141** | **149,090,259** | **274,943,401** | **278,193,360** |
| **Net assets** | | **77,391,754** | **39,156,156** | **116,547,910** | **72,163,301** |
| **SHAREHOLDER'S EQUITY** | | | | | |
| Share capital | 24 | 1,531,456 | 1,413,674 | 2,945,130 | 2,945,130 |
| Fair value reserve | 26 | 938,080 | 23,362,001 | 24,300,081 | 22,682,812 |
| Other reserves | 26 | - | 638,608 | 638,608 | 638,608 |
| Revaluation reserve | 26 | 23,173,753 | 12,950,392 | 36,124,145 | 36,039,330 |
| Retained earnings/(Accumulated losses) | 26 | 32,487,072 | - | 32,487,072 | (266,360) |
| Contingency reserve | 25 | 19,261,393 | 791,481 | 20,052,874 | 10,123,781 |
| **Total shareholder's equity** | | **77,391,754** | **39,156,156** | **116,547,910** | **72,163,301** |

The financial statements were approved and authorized for issue by the Board of Directors on................................ and signed by:

Laston T. Msongole, **Chairperson** — Dr. Elirehema J. Doriye, **Managing Director** — Dr. Joseph S. Kiria, **Director**

## STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHESIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| Details | Note | General insurance | Life assurance | Total | Total |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2020/21 | 2020/21 | 2020/21 | 2019/20 |
| | | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 |
| Gross written premium | 27 | 74,631,861 | 12,769,673 | 87,401,534 | 72,189,479 |
| Written premium ceded to reinsures | 28 | (29,906,006) | - | (29,906,006) | (26,713,865) |
| **Net written premium** | | **44,725,855** | **12,769,673** | **57,495,528** | **45,475,614** |
| Change in gross provisions for unearned premium | 31 | 6,881,151 | - | 6,881,151 | 9,054,455 |
| **Net earned premium** | | **51,607,006** | **12,769,673** | **64,376,679** | **54,530,069** |
| Commission income from re-insurance | 29 | 5,345,559 | - | 5,345,559 | 9,787,506 |
| Finance and investment income | 32(i) | 765,349 | 3,608,538 | 4,373,887 | 10,279,698 |
| Interest income | 32(ii) | 10,594,879 | 1,904,772 | 12,499,651 | - |
| Other operating income | 33 | 12,792,191 | 14,954,713 | 27,746,904 | 1,848,118 |
| **Total income** | | **81,104,984** | **33,237,696** | **114,342,680** | **76,445,391** |
| Claims and policyholders' benefits incurred | 34 | (6,655,091) | (17,775,211) | (24,430,302) | (29,330,111) |
| Reinsurers' share of claims and benefits incurred | 30 | 7,884,097 | - | 7,884,097 | 11,239,087 |
| **Net policyholders' claims and benefits incurred** | | **1,229,006** | **(17,775,211)** | **(16,546,205)** | **(18,091,024)** |
| Acquisition costs | 10 | (951,456) | (859,676) | (1,811,132) | (1,926,598) |
| Administrative expenses | 35 | (12,202,573) | (6,235,135) | (18,437,708) | (20,664,654) |
| Impairment losses | 36 | (4,157,508) | (402,094) | (4,559,602) | (2,815,054) |
| **Total operating expenses** | | **(16,082,531)** | **(25,272,116)** | **(41,354,647)** | **(43,497,330)** |
| **Operating profit/(loss)** | | **65,022,453** | **7,965,580** | **72,988,033** | **32,948,061** |
| Finance costs | 37 | (47,456) | (17,285) | (64,741) | - |
| Share of profit of equity-accounted investees, net of tax | 38 | - | 177,308 | 177,308 | 706,303 |
| **Profit/(loss)before taxation** | | **64,974,997** | **8,125,603** | **73,100,600** | **33,654,364** |
| Tax expense | 39 | (15,968,017) | - | (15,968,017) | (11,180,935) |
| Transfer to policyholders' fund | | - | (8,125,603) | (8,125,603) | (1,474,387) |
| **Profit/(loss) for the year** | | **49,006,980** | - | **49,006,980** | **20,999,042** |
| **Other comprehensive income:** | | | | | |
| Fair value (loss)/gains on equity securities net of deferred tax | | 232,620 | 1,384,649 | 1,617,269 | (125,156) |
| **Total comprehensive income for the year** | | **49,239,600** | **1,384,649** | **50,624,249** | **20,873,886** |

The financial statements were approved and authorized for issue by the Board of Directors on.................................... and signed by:

Laston T. Msongole, **Chairperson** — Dr. Elirehema J. Doriye, **Managing Director** — Dr. Joseph S. Kiria, **Director**

## COMBINED STATEMENT OF CHANGE IN EQUIRY FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Share capital | Fair value reserves | Other reserves | Revaluation reserve | Accumulated (losses)/retained earnings | Contingency reserve | Total equity | Life fund |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 |
| **Balance at 01 July 2020** | **2,945,130** | **22,682,812** | **638,608** | **36,039,330** | **(266,360)** | **10,123,781** | **72,163,302** | **99,582,068** |
| Prior year adjustment* | - | - | - | 84,815 | (6,452,152) | - | (6,367,337) | (203,994) |
| **Balance at 01 July 2020 (restated)** | **2,945,130** | **22,682,812** | **638,608** | **36,124,145** | **(6,718,512)** | **10,123,781** | **65,795,964** | **99,378,074** |
| **Total comprehensive income for the year:** | | | | | | | | |
| Profit for the year | - | - | - | - | 49,006,980 | - | 49,006,980 | - |
| Surplus for the year transferred to policyholders' fund | - | - | - | - | - | - | - | 8,125,603 |
| **Other comprehensive income:** | | | | | | | | |
| Revaluation of Investment Property net of deferred tax | - | - | - | | - | - | | - |
| Revaluation of PPE net of deferred tax | - | - | - | | - | - | | - |
| Fair value gain on equity securities net of deferred tax | - | 1,617,269 | - | - | - | - | 1,617,269 | - |
| **Total comprehensive income for the year** | - | **1,617,269** | | | **49,006,980** | - | **50,624,249** | **8,125,603** |
| Transfer to contingency reserve | - | - | - | - | (9,801,396) | 9,929,093 | 127,697 | (127,697) |
| **Balance at 30 June 2021** | **2,945,130** | **24,300,081** | **638,608** | **36,124,145** | **32,487,072** | **20,052,874** | **116,547,910** | **107,375,980** |

The financial statements were approved and authorized for issue by the Board of Directors on.............................. and signed by:

Laston T. Msongole, **Chairperson** — Dr. Elirehema J. Doriye, **Managing Director** — Dr. Joseph S. Kiria, **Director**

## STATEMENT OF CHANGES IN EQUIRY FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021 (Continued)

**Life Assurance business**

| | Share capital | Fair value reserves | Other reserves | Revaluation reserve | Contingency reserve | Total equity | Life fund |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 |
| **Balance at 1 July 2020** | **1,413,674** | **21,977,352** | **638,608** | **13,336,717** | **663,784** | **38,030,135** | **99,582,068** |
| Prior year adjustments* | | | - | **(386,325)** | | **(386,325)** | (203,994) |
| **Balance at 1 July 2020 (restated)** | **1,413,674** | **21,977,352** | **638,608** | **12,950,392** | **663,784** | **37,643,810** | **99,378,074** |
| **Total comprehensive income for the year:** | | | | | | | |
| Deficit for the year transferred to policyholders' fund | - | - | - | - | - | - | 8,125,603 |
| **Other comprehensive income:** | | | | | | | |
| Revaluation of Investment Property net of tax | - | - | - | - | - | - | - |
| Revaluation of property and equipment net of deferred tax | - | - | - | - | - | - | - |
| Fair value gain on equity securities net of deferred tax | | 1,384,649 | | | | 1,384,649 | - |
| **Total comprehensive income** | - | 1,384,649 | - | - | - | 1,384,649 | 8,125,603 |
| Transfer to contingency reserve | - | - | - | - | 127,697 | 127,697 | (127,697) |
| **Balance at 30 June 2021** | **1,413,674** | **23,362,001** | **638,608** | **12,950,392** | **791,481** | **39,156,156** | **107,375,980** |

*The prior year adjustment is the result of the recognition of assets of TZS 386,325,038.61; depreciation of TZS 203,994,552.59 due to use of replacement cost instead of depreciated replacement cost. Also, there is TZS 1,384,648,958.3 which is made up of fair value gain on Equity Investments amounting TZS 1,978,069,940.42 deducted by deferred tax amounting TZS 593,420,982.13.

The financial statements were approved and authorized for issue by the Board of Directors on.................................2022 and signed by:

Laston T. Msongole, **Chairperson** — Dr. Elirehema J. Doriye, **Managing Director** — Dr. Joseph S. Kiria, **Director**

## STATEMENT OF CHANGES IN EQUIRY FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021 (Continued)

**General insurance business**

| | Share capital | Fair value reserves | Revaluation reserve | Accumulated losses | Contingency reserve | Total equity |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 |
| **Balance at 1 July 2020** | **1,531,456** | **705,460** | **22,702,613** | **(266,360)** | **9,459,997** | **34,133,166** |
| Prior year adjustments* | - | - | 471,140 | (6,452,152) | - | (5,981,012) |
| **Balance at 1 July 2020 (restated)** | **1,531,456** | **705,460** | **23,173,753** | **(6,718,512)** | **9,459,997** | **28,152,154** |
| **Total comprehensive income for the year:** | | | | | | |
| Profit for the year | - | - | - | 49,006,980 | - | 49,006,980 |
| | - | - | - | - | - | - |
| Other comprehensive income: | | | | | | |
| Revaluation of Investment Property net of tax | - | - | | | | |
| Revaluation of property and equipment net of deferred tax | - | - | | - | - | - |
| Fair value loss on equity securities net of deferred tax | - | 232,620 | - | - | - | 232,620 |
| **Total comprehensive income** | | **232,620** | | **49,006,980** | - | **49,239,600** |
| Transfer to contingency reserve | - | - | - | (9,801,396) | 9,801,396 | - |
| **Balance at 30 June 2021** | **1,531,456** | **938,080** | **23,173,753** | **(32,487,072)** | **19,261,393** | **77,391,754** |

*Prior year adjustments is the result of recognition of assets of TZS 471,140,001.28 initially not reflected in financial year ended 30 June 2020.Furthermore, it includes the adjustments made on retained earnings as result of recognition of depreciation of TZS 1,500,689,344 (due to use of replacement cost instead of depreciated replacement cost); investment property (due to non-recognition) of TZS 37,500,000.00; Value Added Tax of TZS 5,052,385,586.00 (due to over booking resulting from internal tax health check audit) and premium levy of TZS 138,423,753.00 (due to overbooking of premium levy expense). Also there is TZS 232,619,929.80 which is made up of fair value gain on Equity Investments amounting TZS 332,314,185.44 deducted by deferred tax amounting TZS 99,694,256.63.

The financial statements were approved by the Board of Directors on....................................2022 and signed by:

Laston T. Msongole, **Chairperson** — Dr. Elirehema J. Doriye, **Managing Director** — Dr. Joseph S. Kiria, **Director**

## STATEMENT OF CASH FLOWS FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Note | General Insurance 2020/21 | Life Assurance 2020/21 | Total 2020/21 | Total 2019/20 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 |
| **CASH FLOWS FROM OPERATING ACTIVITIES** | | | | | |
| Premium received | 49 | 84,604,464 | 12,808,361 | 97,412,825 | 83,575,888 |
| Unearned premium, | 49 | 6,881,151 | - | 6,881,151 | 13,805,904 |
| Commission and Claims received from reinsurers | 49 | 8,351,378 | - | 8,351,378 | 20,279,305 |
| Receipts from Miscellaneous Income | 49 | (1,581,365) | 20,703,346 | 19,121,981 | (22,085,277) |
| Premium paid to reinsurers | 49 | (26,182,152) | - | (26,182,152) | (32,798,802) |
| Gratuity Paid | | (363,664) | - | (363,664) | (67,612) |
| Claims Paid | 49 | (10,087,981) | (11,524,624) | (21,612,605) | (13,179,297) |
| Commission and Administrative expense paid | 49 | (22,754,428) | (7,143,989) | (29,898,417) | (14,504,947) |
| Corporate Tax Paid | 39B | (13,610,271) | - | (13,610,271) | (11,863,606) |
| Value Added Tax Paid | 49 | (13,219,054) | (2,330,150) | (15,549,204) | |
| **Net cash flows from/(used) operating activities** | | **12,038,078** | **12,512,944** | **24,551,022** | **23,161,556** |
| **CASH FLOWS FROM INVESTING ACTIVITIES** | | | | | |
| Purchase of Property and Equipment | 4 | (57,417) | (340,606) | (398,023) | (858,741) |
| Purchase of Intangible Assets | 8&9 | (204,364) | (17,325) | (221,689) | (9,668) |
| Proceeds from Investment Income | 49 | 8,998,216 | 3,200,386 | 12,198,602 | 10,279,699 |
| Rehabilitation of Investment Property | | - | (39,742) | (39,742) | - |
| Investment in Treasury Bonds | 49 | (34,270,870) | (26,239,388) | (60,510,258) | (47,589,874) |
| Investment in Treasury Bills | 49 | (866,850) | 580,325 | (286,525) | 952,498 |
| Investment in Call | 49 | 4,708,413 | 1,465,787 | 6,174,200 | (4,349,295) |
| Investment in Fixed Deposit | 49 | 6,933,752 | 2,206,876 | 9,140,628 | (9,123,388) |
| **Net cash generated from/ (used in) investing activities** | | **(14,759,120)** | **(19,183,687)** | **(33,942,807)** | **(50,698,769)** |
| | | | | | |
| **Increase/(Decrease) in Cash and Cash equivalent** | | **(2,721,042)** | **(6,670,743)** | **(9,391,785)** | **(27,537,213)** |
| **Cash and Cash equivalent at start of the year** | | **22,572,933** | **2,720,521** | **25,293,454** | **52,830,667** |
| **Cash and Cash equivalent at the end of the year** | | **19,851,891** | **(3,950,222)** | **15,901,669** | **25,293,454** |

The financial statements were approved by the Board of Directors on.......................... 2022 and signed by:

Laston T. Msongole, **Chairperson** — Dr. Elirehema J. Doriye, **Managing Director** — Dr. Joseph S. Kiria, **Director**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe udhibiti kasi vifo vya wanyamapori

**RIPOTI** ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), pamoja na mambo mengine imebaini vifo vya wanyamapori 614 kutokana na ajali za barabarani katika kipindi cha mwaka mmoja, sawa na vifo vya wanyamapori 51 kwa mwezi.

Pia, CAG Charles Kichere alibainisha takwimu hizo katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 aliyoikabidhi kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Machi 30, mwaka huu na kuwasilishwa bungeni jijini Dodoma Aprili 12, mwaka huu.

Alisema Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) linasimamia jumla ya hifadhi 22 zenye ukubwa wa kilomita za mraba 104,170 na kati yake ni Hifadhi za Taifa Mikumi, Serengeti, Tarangire na Ziwa Manyara.

CAG alisema Hifadhi ya Taifa ya Mikumi inapitiwa na barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 45 huku Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ikipitiwa na barabara ya changarawe yenye urefu wa kilomita 12 ikitokea Mbalageti hadi Mto Robana.

Kwa mujibu wa CAG, mwaka 2020/21, wanyama 535 waliuawa kwenye ajali za barabarani katika Hifadhi ya Taifa Mikumi kulinganishwa na wanyama 106 katika mwaka 2019/20.

Idadi hiyo ni ongezeko la wanyama 429, sawa na asilimia 405, huku wanyama 50 waliuawa katika Hifadhi ya Taifa Serengeti; wanyama 18 waliuawa Hifadhi ya Taifa Tarangire; na wanyama 11 waliuawa Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara.

Kwa maoni yake, ikiwa hatua madhubuti za usalama hazitachukuliwa kuzuia uzembe wa madereva ndani ya barabara zinazopita kwenye hifadhi za taifa, kuna uwezekano wa wanyamapori kuendelea kuuawa kwa ajali za barabarani.

Alipendekeza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), kupitia upya taratibu za uendeshaji salama wa magari ndani ya hifadhi za taifa nchini ili kudhibiti ajali zinazoua wanyamapori hifadhini.

Idadi ya wanyamapori waliouawa ni hasara kwa taifa kwa kuwa uwapo wao unawezesha taifa kupata fedha za kigeni, kupitia watalii wanaokuja kwa ajili ya kuwaona.

Ni lazima wanyama watembee kutoka eneo moja kwenda jingine ndiyo maana kuna maeneo ya mtawanyiko na mapito ya wanyama maarufu kama shoroba. Wanyamapori hutembea kutoka eneo moja hadi jingine kutafuta mahitaji muhimu kama udongo wenye madini, majani na maji, wengine kama nyumbu huwa na maeneo maalumu ya kuzalia ambayo husaidia ndama wao kupata chakula.

Ili Hifadhi za Taifa na maeneo yaliyohifadhiwa yawepo ni lazima kuwe na mapito ya wanyama ambayo yanapaswa kulindwa vinginevyo watabaki kwenye kisiwa na kuna uwezekano mkubwa aina ya wanyamapori kupotea au kuzaliana wao kwa wao ambao ni ndugu hali inayosababisha ugonjwa ukiingia ni rahisi kufa kwa pamoja au kupata aina inayodumaa kwa kuwa hakuna mchanganyiko kwenye uzazi.

Ili wanyamapori waendelee kuwapo ni lazima kutunza ikolojia ya maeneo husika inayowalinda, kuzaliana na kukua bila tatizo ili mtalii anapofunga safari kutoka Ulaya, Marekani na China kwa ajili ya kuona simba, tembo, faru, chui, twiga na wengine awaone bila kikwazo.

Katika maeneo yote yaliyopitiwa na barabara kuna alama za barabarani zinazoonyesha eneo husika linapitiwa na wanyamapori, dereva anapaswa kuendesha kwa uangalifu mkubwa, lakini bado wameendesha kwa kasi hususan nyakati za usiku.

Barabara ya Mikumi-Morogoro kuna mabango yanayoonyesha gharama za kila mnyama atakayegongwa na kuwataka madereva kuendesha kwa kuzingatia vibao, lakini hawafanyi hivyo matokeo yake wanyama wanapotea kama CAG alivyobainisha.

Ni lazima kuchukua hatua madhubuti kama ni kuongeza matuta, kuweka kamera ya kutambua magari yanayogonga wanyama na kuchukua hatua au kuondoa barabara hizo.

Bila kuweka utaratibu wa kulinda rasilimali hii, kusikiliza na kutekeleza ushauri wa CAG, huku kukiwa na ongezeko la watu, ni wazi itafika wakati maeneo yaliyohifadhiwa yatabaki machache hali itakayopunguza watalii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Elimu zaidi kwa umma kuhusu sensa itaepusha upotoshaji

Na Sabato Kasika

**AGOSTI** 23 mwaka huu itakuwa ni siku ya Sensa ya Watu na Makazi nchini, ambayo msingi wake ni serikali kupata takwimu za idadi ya Watanzania, ili ziisaidie kupanga mipango ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wake.

Tangu mwaka jana ulipoanza mchakato wa sensa hiyo, yamesemwa mengi na baadhi ya Watanzania ambayo ninadhani ipo haja ya kuongeza kasi ya utoaji wa elimu ili watu wawe na uelewa wa kutosha kuhusu sensa.

Kwa nini? Wapo baadhi ya watu wamekuwa wakidai kwamba kwenye sensa kuna dodoso la yasiyohusiana, jambo ambalo wakati mwingine linaweza kuleta mkanganyiko.

Ninakumbuka Rais Samia Suluhu Hassan, alishalitolea ufafanuzi kuwa hayo potofu hayapo, lakini huko mitaani na vijiweni, wapo baadhi ya watu wamekuwa wakilizungumzia wakidai kuwa lipo dodoso la aina hiyo.

Wakati kukiwa na madai kama hayo, wengine wamekuwa wakihusisha sensa hiyo na chanjo ya UVIKO-19, kwamba inalenga kujua idadi ya Watanzania waliochanjwa na wale ambao hawajachanjwa.

Kuna wakati Kamisaa wa Sensa, Anne Makinda alilikemea hilo na kuwataka watu waache imani potofu na kufafanua kwamba sensa haihusiani na chanjo hiyo ingawa ni muhimu kupata chanjo.

Hivyo kwa hali kama hiyo, ni vyema wakati huu wa kuelekea kwenye sensa, kasi ya utoaji wa elimu ikaongezeka ili kuhakikisha watu wanaachana na upotoshaji huo ambao unaweza kusababisha baadhi ya watu wasihesabiwe.

Kama watoaji elimu watakuwa ni wachache, basi si vibaya idadi ikaongezwa ili kuharakisha kazi hiyo kwa umma wa Watanzania kwa lengo la kuepusha upotoshaji unaoendelea mitaani.

Ninaamini kwamba kwa jinsi ambavyo maandalizi ya sensa yanavyoendelea, ikiwamo kutumia utaratibu wa anwani za makazi, mpango shirikishi ulioandaliwa kati ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar wa kutekeleza kazi hiyo unaweza kusaidia, iwapo Watanzania wataelimishwa vya kutosha na kuachana na elimu nyingine ambazo wamekuwa wakipandikiziwa.

Kwa kuwa itaonyesha ni wapi kila mwananchi anapoishi, itasaidia pia serikali kupanga mipango ya maendeleo, kuimarisha usalama, kuongeza ajira na mapato ya serikali.

Serikali hutumia sensa ili kujua jinsi ya kupanga na kukadiria matumizi ya rasilimali na fedha, pia wanasiasa hutumia idadi ya watu na maeneo walioko kutathmini azma zao za kisiasa.

Hayo mengine yanayoenezwa mitaani kwamba inalenga kujua idadi ya Watanzania waliochanjwa au suala la dini, yasingepewa nafasi kama jamii itapewa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa sensa.

Kuwapo mkanganyiko huo ndani ya jamii, ni wazi kwamba bado wapo baadhi ya Watanzania ambao hawajajua umuhimu wa sensa, ingawa imekuwapo tangu mwaka 1963.

Ikumbukwe kuwa serikali inaweza kushindwa kupanga shughuli zake za maendeleo iwapo haitakuwa na takwimu sahihi za idadi ya Watanzania, hivyo ninadhani ni muhimu kila Mtanzania kuhesabiwa.

Hiyo inaweza kufanikiwa iwapo wote tutakuwa na kauli moja kwamba tuwe tayari kuhesabiwa Agosti 23 badala ya kuwapo wengine wanaopenyeza elimu nyingine yenye lengo la kukwamisha sensa.

Watu wenye mawazo hayo ni vyema wakakumbushwa kuwa bila idadi ya Watanzania kujulikana, ni vigumu kwa serikali kufanikisha malengo ambayo imejiwekea ya kuwahudumiwa wananchi wake.

Pamoja na hayo, ni muhimu kutambua kuwa si kuhesabiwa tu, bali pia wajibu wa kila Mtanzania kutoa maelezo sahihi yanayomhusu, ambayo kimsingi ndiyo serikali inachohitaji.

Iwapo kutakuwa na mtu ambaye amejipanga kutoa taarifa za uongo kwa sababu ya kuhofia suala la udini au chanjo, ni wazi lengo la sensa halitatimia na pia atakuwa ameikwamisha serikali yake.

Nimalizie kwa kurudia kuwa, ni wakati sasa wa kuendelea kutoa elimu zaidi kwa umma, ili utambue na kuepuka ushawishi mwingine wa mitaani wenye lengo la kukwamisha sensa hiyo.

## Serikali yawapa neno walezi wa watoto wenye mahitaji maalum

**Peter Haule na Saidina Msangi,** DODOMA

Serikali imewataka walezi wa watoto wenye mahitaji maalumu kufanya kazi hiyo kwa bidii na kwa upendo kwa kuwa wanalisaidia Taifa katika kuwapatia elimu, maadili na kupunguza watoto wa mitaani.

Ushauri huo ulitolewa jijini Dodoma na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Huduma za Hazina, Jenifa Omolo, wakati Wizara yake na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango walipotoa misaada yenye thamani ya Shilingi milioni tisa, vyakula na vinywaji katika Vituo vya Watoto wenye mahitaji maalumu vya Rahma, Cheshire na Matumaini.

Omolo alisema kuwa kazi zinazofanywa katika vituo hivyo serikali inazitambua kwa kuwa ni kazi zinazohitaji upendo mkubwa ambao Mungu ameweka katika mioyo ya walezi wa watoto hao.

"Msaada huu tumeutoa kama Wizara kwa kutambua umuhimu wenu kwa kuwa watoto hao msinge wakusanya hapa inawezekana wasingepata nafasi ya kulelewa na kupata elimu na maadili mema, ikizingatiwa kuwa hawa ni viongozi wa kesho," alieleza Omolo.

Alisema lengo la Wizara yake ni kufurahi pamoja na kuwatia moyo kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kuwasaidia watoto katika mahitaji yao ambayo wangeyapata kwa wazazi wao.

Aidha, aliupongeza uongozi wa vituo hivyo kwa kazi kubwa wa kuwalea watoto na kuwataka waendelee kuwa mama na baba kwa kuwafundisha elimu ya dini na kupata masomo mengine yatakayo waongezea ujuzi na maarifa.

Aliwaasa watoto katika vituo hivyo kuwa waadilifu, wasikivu kwa walezi wao na kuzingatia masomo.

Mlezi wa Kituo cha Rahma, Rukia Khamis Abdalah, aliishukuru Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar kwa kitendo hicho cha kutoa misaada ambacho amekitaja kuwa ni ibada kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na wamefanya biashara na Mwenyezi Mungu na atawalipa baada ya maisha ya hapa Duniani

Mlezi wa Kituo cha Matumaini Sista Maria Peter, amesema kuwa watoto wanaolelewa katika kituo chake wanapatikana kupitia maofisa ustawi wa jamii, ambapo maofisa hao wanapopata watoto wanatoa taarifa na kuomba nafasi ya kuwalea katika kituo, pia ameshukuru kwa msaada huo kwa kuwa watoto wanafarijika kwa kuuona upendo.

# TIC yasajili miradi 85 itakayotoa ajira 12,191

**Na Mwandishi Wetu**

Katika kuhamasisha uwekezaji nchini na kuchochea uwekezaji na ukuaji wa uchumi Kituo cha Uwekezaji cha (TIC) kimesajili miradi 85 tangu Januari hadi Machi mwaka huu ambayo itasadia katika kuzalisha ajira na kukuza pato la Taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Dk. Maduhu Kazi alisema kiwango hicho ni kikubwa kulinganisha na idadi ya miradi 51 kwa kipindi cha mwaka 2021 ambapo ajira 12,191 zinatarajiwa kuzalishwa.

"Miradi hiyo ina thamani ya Dola za Marekani milioni 787.40 ikilinganishwa na kipindi hicho mwaka 2021 ambapo thamani ya miradi ilikuwa dola milioni 450.56 sawa na ongezeko la asilimia 74.76," alibainisha.

Alisema miradi hiyo imelenga katika uwekezaji kwenye sekta ya usafirishaji, viwanda, miundombinu, kilimo ujenzi/majengo ya biashara, taasisi za fedha, rasilimali watu, utalii na huduma mbalimbali.

Alitaja baadhi ya kampuni zilizowekeza nchini ni Taqa Arabia Tanzania Ltd itakayojenga vituo 12 vya ubadilishaji wa magari kutoka kutumia petroli na dizeli kwenda kwenye mfumo wa gesi na utekelezaji wa vituo viwili vikubwa utakamilika mwaka huu.

"Mradi wa ujenzi wa viwanda vya saruji utatekelezwa na kampuni ya Alotaibnad Blak Bib na Prime Cement wenye thamani ya dola milioni 113 ambapo ajira 1,097 zinatarajiwa kuzalishwa kupitia mradi huo," alisema Dk. Maduhu.

Pia upo wa kuunganisha magari aina ya Howo utakaotekelezwa na kampuni ya Saturn Corporation ambapo kampuni hiyo ni ushirikiano katika ya Tanzania na Canada.

"Katika kuhakikisha upungufu wa mafuta unapungua au kuisha nchini, tumesajili kampuni ya Organo Africa ambayo itakwenda kufanya uzalishaji wa mafuta ya kula tani 182,000 kwa mwaka na kugharimu dola za Marekani milioni 42.68," alisema.

Alieleza kuwa kiwanda hicho kitazalisha ajira za moja kwa moja 1,097 na kutengeneza soko kwa mazao mbalimbali ya wakulima nchini yatakayotumika kama malighafi ya kutengeneza bidhaa hiyo.

Aidha Dkt.Maduhu alisema katika kipindi hicho pia wametiliana saini miradi 6 inayotarajiwa kuwekeza Dola za Marekani bilioni 1.1 ambapo itakwenda kutumika kukuza miradi iliyopo na kuanzisha miradi mipya ukiwemo wa ujenzi wa kiwanda cha mbolea cha Intracom kinachojengwa jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa Dk. Maduhu, TIC itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali katika kuibua fursa na kuzitangaza kwa lengo la kuchochea uwekezaji nchini.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani wakiwa kwenye kituo cha mabasi ya Makambako mkoani Njombe kwa ajili ya ukaguzi wa mabasi kabla hayajaanza safari juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Prof Ngowi alivyozungumzia uchumi wa buluu

**Na Jenifer Gilla**

MWAKA mmoja uliopita, Mhadhiri wa Uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Hayati Prof. Honest Ngowi, alialikwa katika Kongamano la Uchumi wa Buluu Zanzibar, kuzungumzia fursa zinazopatikana kwenye eneo hilo.

Alisema uchumi wa buluu ni utumiaji endelevu wa rasilimali za bahari kiuchumi, ikiwamo uvuvi, kutengeneza vizimba vya kuuzia samaki, kutengeneza majokofu ya kuhifadhia samaki ili kuongeza ubora wa maisha.

Prof. Ngowi alisema kuwa uchumi wa buluu ni moja ya jukwaa lenye kuleta maendeleo ambayo ndani yake kuna mambo mengi ikiwamo viwanda, kilimo na madini ambayo huleta ajira kwa watu na kusaidia kuondoa umaskini.

Alisema jukwaa kama la uchumi wa buluu sio kitu kipya, suala la msingi la kujiuliza ni je, jamii inalitumiaje jukwaa hilo? Lisipotumiwa vizuri itakuwa ni historia tu kuwa kulikuwapo na kitu fulani katika jamii, lakini likitumiwa vizuri inakuwa ni hazina endelevu.

Alisema siku zote fursa huwa hazimfuati mtu na jamii inapaswa kuzitafuta kutoka sehemu mbalimbali, ikiwamo uchumi wa buluu na kuzitendea haki kwa maana ya kuwekeza huko ili kujiongezea kipato na kupunguza kasi ya umaskini.

Akizungumzia fursa zinazopatikana katika sekta hiyo, alisema ni pamoja na kulisha watu wanohusika na biashara ya samaki wakiwamo mama ntilie.

Alitoa mfano wa Mafya ambako shughuli za uvuvi zimeshamiri na kusema kuwa hata wale wanaohusika kuwapikia chakula wavuvi katika viwanda vya samaki wapo katika mnyororo wa uchumi wa buluu.

Fursa nyingine latika uchumi wa buluu anaitaja kuwa ni utengenezaji wa barafu za kuhifadhia samaki, ambayo barafu moja huuzwa kwa Sh. 500 hadi 2,000. Mtu akiweza kuuza dumu 10 kwa siku ana uhakika wa kuingiza Sh. 5,000 hadi 20,000.

Kilimo cha zao la mwani kinatajwa kuwa fursa nyingine kwamba kuanzia kuuza pembejeo na mbegu, kulima, kuchakata na pia kuuweka kwenye makasha (parcKaging) na hata huduma za ugavi, zote ni fursa zinazoweza kumwingizia mtu kipato.

Fursa nyingine kwa mujibu wa Prof. Ngowi ni shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo, ikiwamo maboti na meli.

Alisema kinachoangaliwa hapo sio vyombo pekee bali hata wanaohusika kuviendesha akiwamo baharia, kapteni, biashara ya vyakula ndani za meli hizo, vyote ni uchumi wa buluu.

Alitaja suala la uvunaji wa viumbe hai waishio baharini kama samaki, ambao hutumika kwa ajili ya chakula, ambalo anahitajika mvuvi, mnunuzi, mkaangaji na mlaji.

Pia, alisema baadhi ya viumbe hao mabaki yao hutumika kutengenezea urembo kama bangili, hereni, cheni na mapambo mengine ya ukutani ambayo hufanya vizuri kwenye masoko ya kitaifa na kimataifa.

Utalii, alisema ni sehemu ya uchumi wa buluu ikiwamo fukwe kutumika kama sehemu ya kupumzikia, hoteli kubwa, vyakula vinavyolisha watalii, zote ni fursa zinazopatikana katika uchumi wa buluu.

# CAG ataja kiini upotevu mapato Sekta ya Madini

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ametaja mambo yanayochangia upotevu wa mapato ya Sekta ya Madini nchini, ukiwamo upungufu mkubwa wa wathaminishaji madini migodini.

CAG Charles Kichere anabainisha dosari hizo katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumanne ya wiki iliyopita.

Anasema ukaguzi wake ulibaini kutokuwapo kwa miongozo kuhusu taratibu za uthaminishaji wa madini ya viwandani, madini ya nishati na madini ujenzi katika kuhakikisha uwapo wa usawa kwenye taratibu za uthaminishaji wa madini.

CAG anafafanua kuwa ilibainika miongozo iliyopo ni ile ya uthaminishaji wa aina moja tu ya madini ambayo ni vito na almasi huku aina zingine za madini kama vile madini ya viwandani, madini ya nishati na madini ujenzi kufanyiwa uthaminishaji pasipo mwongozo au utaratibu sahihi.

Hata hivyo, CAG anasema ilibainika kuwa miongozo katika uthaminishaji wa madini ya metali ilitolewa katika mwaka wa fedha 2021/22, hali inayomaanisha kuwa kwa kipindi cha miaka ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/21, Tume ya Madini haikuwa na miongozo ya uthaminishaji wa madini ya metali.

"Aidha, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa uthaminishaji wa madini ya almasi/vito haukujitosheleza kwa maana ya uwapo wa idadi ya wathaminishaji wachache kulingana na matakwa na viwango vya miongozo husika.

"Ukaguzi wangu ulibaini ofisi tano za maofisa madini wa mikoa ya Singida, Mahenge, Lindi, Morogoro na Tunduru zimekuwa na wathaminishaji wa madini chini ya wawili, na ofisi zingine saba zikiwa na wathaminishaji wasiopungua wawili.

Pia ilibainika kumekuwa na usimamizi usioridhisha katika kusimamia ubora na wingi wa madini yanayopatikana kutokana na kutokuwapo kwa mgawo wa kutosha wa maofisa migodi wakazi kwenye maeneo ya uzalishaji madini.

"Ilibainika zaidi kuwa uthaminishaji wa wingi wa madini ya viwandani kwa kiasi kikubwa unategemea wingi wa kiasi cha madini kinachowasilishwa na wamiliki wa leseni husika na hakuna utaratibu wowote unaotumika kujiridhisha kuhusu kiasi kinachowasilishwa.

"Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa kuwapo kwa utaratibu usiojitosheleza wa uthaminishaji wa madini kumechangiwa na kutokuweka kipaumbele kwenye kusisitiza uzingatiaji wa taratibu zinazopaswa kufuatwa wakati wa uthaminishaji wa aina zote za madini.

"Kama sehemu ya ufuatiliaji wa mapato yanayopaswa kulipwa, ilibainika kuwa Tume ya Madini kupitia ofisi za maofisa madini wakazi imekuwa ikidhibiti kiasi cha madini yanayopatikana katika migodi mikubwa na ya kati kwa kuwatumia maofisa migodi wakazi.

Vilevile, CAG anabainisha kuwa kumakuwapo na jumla ya maofisa migodi wakazi 13 kulinganishwa na idadi ya kampuni za uzalishaji wa madini 287 zilizopo.

CAG anafafanua zaidi kwamba mapitio ya idadi ya maofisa migodi wakazi waliopo katika Tume ya Madini yameonyesha kwamba wengi wao walikuwa wamepangiwa kazi katika maeneo yanayochimba dhahabu (7 kati ya 13).

Hata hivyo, CAG anasema mahojiano na maofisa katika Tume ya Madini yalibainisha kwamba maofisa wengi walipangiwa kazi katika maeneno yaliyokuwa na hatari kubwa zaidi ya upotevu wa mapatao ingawa eneo la kiwanda kama Dangote halikuwa na ofisa madini mkazi.

"Hivyo, upungufu uliobainishwa kwenye taratibu za uthaminishaji wa madini unaashiria uwezekano wa ukadiriaji wa chini kwenye uwasilishaji wa kiasi cha madini yanayopatikana kwani kiasi hicho ni mojawapo ya vigezo katika kubainisha tozo zinazopaswa kulipwa serikalini," CAG anatahadharisha.




Baadhi ya wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari wilayani Temeke mkoani Dar es Salaam wakiwa kwenye kampeni ya kupinga rushwa ya ngono shuleni mwishoni mwa wiki, iliyoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI). **PICHA: SABATO KASIKA**

## Sita wazaliwa mkesha pasaka hospitali rufani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATOTO sita wamezaliwa katika mkesha wa Pasaka Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, huku watatu wakizaliwa kwa njia ya upasuaji na mmoja akiwa na uzito pungufu.

Ofisa Muuguzi kiongozi wodi ya wazazi katika hospitali hiyo, Experantia Misalaba, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari vilipotembea hospitali hapo.

Alisema katika mkesha huo walifanikiwa kupata watoto sita na watatu walizaliwa kwa njia ya upasuaji, lakini wototo watano afya zao zinaendelea vizuri.

"Watoto hawa sita ambao wamezaliwa kwenye mkesha wa Pasaka hospitalini hapa, wa kike ni watano na wakiume mmoja na afya zao ni nzuri, kasoro huyu mmoja ambaye amezaliwa akiwa na uzito pungufu," alisema Misalaba.

Aidha, alitoa wito kwa wajawazito mkoani humo wawe wanahudhuria kliniki mara kwa mara, ili kufahamu maendeleo ya mtoto tumboni, pamoja na kujifungulia kwenye huduma za afya sehemu ambazo ni salama na kuepuka vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi.

Baadhi ya kinamama ambao walijifungua watoto kwenye mkesha huo walishukuru kujifungua salama na kutoa wito kwa wenzao hasa wa maeneo ya vijijini, wajenge tabia ya kujifungua kwenye huduma za afya.

# Wanyamapori 50 wafa shoroba Kwakuchinja

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

UKIUKWAJI wa Sheria za Usalama Barabarani kwa madereva wanaotumia barabara ya Babati-Arusha umesababisha wanyama 50 kufa wanaopita shoroba ya Kwakuchinja inayounganisha Hifadhi ya Taifa Tarangire na Manyara mkoani humo.

Kutokana na matukio hayo serikali imeombwa kuchukua hatua za haraka, ili kuokoa wanyama wanaogongwa na magari katika hifadhi hizo.

Kauli hiyo imetolewa na meneja miradi wa shirika lisilo la kiserikali linajishughulisha na uhifadhi na jamii la Chemchem Safari, Walter Pallangyo, wakati akiwasilisha mada kuhusu nafasi ya sekta binafsi kusaidia uhifadhi wa maliasili kwenye mafunzo yaliyotolewa kwa njia ya mtandao kwa waandishi wa habari za mazingira.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), kupitia mradi wa Tuifadhi Maliasili unafadhiliwa na Shrika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Marekani (USAID).

Alisema kuwa vifo vya wanyama hao 50 vilitokea katika kipindi cha mwaka 2019 vikisababishwa na matukio 380 ya ajali za katika barabara hiyo kutokana na madereva kukiuka sheria za uhifadhi na kwamba endapo serikali haitachukua hatua za makusudi kudhibiti hali hiyo idadi hiyo itaendelea kuongezeka.

Pallangyo alisema kuwa katika utafiti waliofanya mwaka 2019 walibaini katika shoroba ya Kwakuchinja ambayo wanyama wanapita kutoka Hifadhi ya Tarangire na Manyara wastani wa matukio mawili ya kugongwa kwa wanyama yanatokea katika barabara hiyo inayopita ndani ya hifadhi.

Alisema wanyama waliokufa ni Twiga, Nyumbu, Pundamilia, Fisi na Swala.

"Hawa wanyama waliogongwa na kufa katika kipindi hicho ni wale wanaosafiri hasa nyakati za usiku wanapopita katika njia zao kutoka eneo moja kwenda lingine kwa kuvuka barabara kuu hiyo ya Arusha-Babati," alisema meneja huyo miradi.

Alisema shirika hilo la Chemchem limekuwa likifanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha linazuia vitendo hivyo vya ajali za wanyama kwa kuzungumza na wadau wa barabara hiyo kuweka alama za njia ya mapito ya wanyama pamoja na kusimamia sheria za barabarani dhidi ya madereva.

Kwa upande wake, Victoria Michael, kutoka Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), akizungumzia kuhusu ushiriki wa sekta hiyo katika uhifadhi wa Maliasili, alisema wamekuwa wakitoa mafunzo maalumu kwa kila sekta binafsi kutenga bajeti maalumu ya uhifadhi wa maliasili hapa nchini.

Alisema sekta binafsi ni moja ya wadau wakubwa katika uhifadhi wa maliasili na hivi sasa wameamua kulivalia njuga suala la ujangili kwa kuwa wanaofanya vitendo hivyo wengi wao wanatoka sekta binafsi ni lazima wapewe elimu ya kuacha vitendo hivyo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema mradi wa Tuhifadhi Maliasili Unafadhiliwa na USAID umelenga kutoa mafunzo maalumu kwa wanahabari yenye lengo la kuwajengea uwezo wa kuandika habari za uhifadhi uwindaji haramu na usafirishaji wa wanyamapori.

Mwenyekiti wa JET, Dk. Ellen Otaru, alisema elimu hiyo itawasaidia pia waandishi wa habari kuandika habari zitakazosaidia jamii zinazozunguka hifadhi kuona umuhimu wa kutunza maliasili zilizopo nchini na washiriki wanatoka Tanzania Bara na Visiwani.

HABARI KITAIFA

# Wakatishwa tamaa na kukosa soko la mboga

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANAUSHIRIKA wa kikundi cha kulima mboga cha 'Tusikate Tamaa Cooperative Society' kilichopo Shehia ya Tumbe Mashariki kisiwani Pemba wamelalamikia kukosekana kwa soko hilo kuwa kunawarudisha nyuma kimaendeleo.

Walisema wamekuwa wakiuza zaidi soko la ndani ingawa wanapata kipato kidogo kutokana na vikundi vingi vya wajasiriamali kujishughulisha na kilimo hicho. Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa kikundi hicho, Bahati Othman, alisema kuwa, waliamua kuanzisha kilimo hicho kwa lengo la kujiletea maendeleo ingawa wamekuwa wakipata kipato kidogo kilichokuwa hakikidhi mahitaji kutokana na ukosefu wa soko la uhakika.

Alisema sababu kuu ya kukosekana kwa soko hilo ni kuwapo kwa wakulima wengi wa zao hilo tofauti na uhitaji wake katika eneo hilo.

Naye, Katibu wa kikundi hicho, Makame Hassan Makame, alisema kuwa, changamoto nyingine inayowakabili ni ukosefu wa vitendea kazi pamoja na maradhi.

"Ikiwa tutauza vizuri tutapata pesa ya kutatua changamoto zetu wenyewe lakini kipato ni kidogo sana, hivyo tukipata fedha ya kujihudumia ndo tunakosa fedha ya kutatua changamoto za kikundi", alisema Katibu huyo.

Aliongeza kuwa, pamoja na changamoto hizo lakini wamepata mafanikio kwa kiasi, kwani kinawasaidia kutatua changamoto zao ndogo ndogo kwenye familia.

"Tunapata kipato cha kujiendesha kimaisha, tunasomesha watoto wetu, tumejiunga kwenye vikundi vya hisa, jambo ambalo linatusaidia kukopa pale tunapopatwa na tatizo", alisema.

Nae Mwekahazina wa kikundi hicho, Asha Kassim Hassan alieleza kuwa, wanahitaji mikopo yenye masharti nafuu, ili wapate kutatua changamoto za kikundi chao kwa kununua vitendea kazi pamoja na kununua dawa za kuulia wadudu wanaoshambulia mazao hayo.

Mjumbe wa kikundi hicho, Asha Hussein Hamad, aliiomba Serikali kuwasaidia katika kila hatua, ili kuhakikisha wanajikwamua na maisha duni, jambo ambalo litaisaidia nchi kupata maendeleo.

"Kila mwananchi atakapokuwa na uwezo wa kujikwamua, maendeo zaidi yatapatikana, kwa sababu kila mmoja atakuwa na uhakika wa chakula na wataendelea kuanzisha miradi mbali mbali kwa lengo la kujipatia kipato," alisema.

# LHRC yagundua ongezeko la ukatili wa vijana kwa wazee

**Na Christina Mwakangale**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimesema kwamba katika Ripoti ya Haki za Binadamu 2021, kimebaini ongezeko la ukatili wa vijana dhidi ya wazee kwa kuwatelekezea wajukuu, kwa madai wapo mijini kutafuta riziki.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, aliyasema hayo hivi karibuni mkoani Dar es Salaam, wakati akizindua ripoti hiyo.

Alisema ripoti kwa upande wa ukatili dhidi ya wazee, kwa mwaka wa 2021, ilibaini wazee wanaendelea kufanyiwa ukatili wa aina mbalimbali, ikiwamo wa kimwili, kijinsia, kutelekezwa, pamoja na kuingiliwa kwa haki za kumiliki mali hasa kutelekezewa wajukuu.

"Wazee wanaendelea kuwa wahanga wakubwa wa kuuawa kwa tuhuma za uchawi. Parricide (watoto kuua mzazi wao), kwa kawaida huhamasishwa na masuala ya urithi wa mali, pia limeibuka suala la wazee kuachiwa wajukuu.

"Vijana wengi wanazaa watoto halafu hawalei wenyewe, wanabeba na kuwapelekea wazazi wao ambao tayari ni wastaafu, hawana kipato chochote, Mzee huyu atamhudumiaje mtoto, huu ni ukatili ambao upo zaidi, vijana wanadai wanatafuta maisha mijini," alisema Anna.

Pia, alisema kwa upande mwingine ripoti ilibaini kukithiri kwa matukio ya kujiua, mauaji kwenye jamii kuongezeka kutokana na sababu tofauti huku kitendo cha kujiua kikiwa zaidi kwa wanaume.

"Dhana na malezi miongoni mwa jamii za Kiafrika hata Tanzania, kwamba mwanaume ni jasiri anayetakiwa kuvumilia kila jambo, ni kati ya sababu ya wao kuendelea kubaki na masuala mazito binafsi, moyoni na baadhi yao kuchukua uamuzi wa kujiua.

"Jamii zetu tunaona mwanaume hulelewa kama jasiri na mbeba majukumu ikilinganishwa na mwanamke. Katika jamii mwanaume halii, ila mwanamke kulia ni sawa, ndio maana utakuta mwanamke akilia kidogo anasaidiwa, ingawa hata mwanaume ni binadamu ameumbwa kama mwanamke," alisema Anna.

Anna alisema sababu kuu pia ni mfumo dume ambao unachangia matukio mengi ya wanaume kuongoza takwimu za kujiua nchini, ikilinganishwa na yale ya wanawake, akisema ripoti ilibaini asilimia 70 ya wanaume walijiua katika kipindi hicho, wengi wao wakiwa vijana.

"Tangu mdogo mtoto wa kiume akilia utasikia anaambiwa mwanaume halii bwana!. Lakini mwanaume huyu pia akija kuwa mtu mzima amekua na dhana hiyo hiyo, jambo ambalo hata akiwa na shida hasemi, anavumilia na hupata msongo wa mawazo," alisema Anna.



Wadau mbalimbali wa zao la ufuta mkoani Lindi wakiwamo viongozi vyama vya msingi (AMCOS) na vyama vikuu vya ushirika wakifuatilia mada mbalimbali wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Jaza Kibubu Uvune' inayoendeshwa na Benki ya NBC mahususi kwa wakulima wa zao hilo mkoani humo wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni yahamasisha kilimo cha ufuta

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

KATIKA jitihada za kuhamasisha kilimo cha zao la ufuta, kampeni maalum imezinduliwa kwa lengo hilo.

Kampeni hiyo imezinduliwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa wakulima wa zao hilo katika mkoa wa Lindi inayofahamika kama 'Jaza Kibubu Uvune' inayolenga kuhamasisha wakulima hao kujiwekea akiba kupitia benki hiyo, huku wakipata fursa ya kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo baiskeli na pikipiki.

Hatua ya benki hiyo imeungwa mkono na serikali kupitia Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, ambae amebainisha kuwa kupitia kampeni hiyo wakulima wa zao la ufuta mkoani Lindi watahamasika zaidi kuwekeza juhudi zao kwenye kilimo cha zao hilo la kimkakati, huku pia wakiendelea kujijengea utamaduni wa kutunza akiba.

Akizungumza kwenye hafla ya uzinduzi wa kampeni hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita mkoani Lindi na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa zao hilo wakiwamo viongozi wa kiserikali, viongozi wa vyama vya msingi (AMCOS) na vyama vikuu vya ushirika pamoja na wakulima, Ndemanga alisema hatua ya benki hiyo inakwenda sambamba na mkakati wa mkoa huo katika kuhamasisha kilimo cha mazao ya kimkakati ikiwamo ufuta na korosho.

"Kwa hapa Lindi, zao la ufuta ni zao la pili kibiashara baada ya korosho na sisi ndio wazalishaji wakubwa wa ufuta hapa nchini. Ujio wa kampeni hii utatusaidia sana kutuwezesha tuendelee kuwa vinara zaidi kwa kuwa sasa wakulima watahamasika zaidi na pia itavutia hata wale ambao sio wakulima wa zao hili nao pia waingie rasmi kwenye kilimo hiki, tunawashukuru sana NBC," alisema

Ndemanga pia alitoa wito kwa wakulima hao kuweka akiba zao kupitia benki hiyo ili wanufaike zaidi.

Ofisa Mkuu wa Uendeshaji Benki ya NBC, Alelio Lowassa, alisema inalenga kuunga mkono maelekezo ya serikali yanayozitaka taasisi za fedha nchini kuwekeza zaidi kwenye kilimo kwa kubuni huduma zinazolenga kumsaidia zaidi mkulima.

"Kupitia kampeni hii wakulima watakaojiwekea akiba kuanzia kiasi cha Sh. 500,000 kwenye akaunti zao za NBC Shambani watakuwa kwenye nafasi ya kujishindia baiskeli na pikipiki kupitia droo zitakazofanyika kila baada ya wiki mbili ndani ya miezi mitatu ya kampeni hii." alibainisha.

Mwenyekiti wa AMCOS ya Tulinde ya wilayani Tandahimba, Mustapha Rashid Salehe, alisema pamoja na kuwahamasisha wakulima wa zao la ufuta kujiwekea akiba kupitia benki hiyo, kupitia kampeni hiyo wakulima hao watahamasika zaidi kuongeza juhudi katika uzalishaji wa ufuta kupitia zawadi mbalimbali zitakazotolewa, ikiwamo baiskeli na pikipiki.

"Naamini kampeni hii itatuongezea sana ari ya kuendelea kulima zao la ufuta kwa sababu tunaamini nyuma yetu tunaungwa mkono na taasisi kubwa za kifedha kama NBC ambayo kupitia kampeni hii itatuwezesha kutunza fedha zetu bila makato yoyote huku pia tukiwa kwenye nafasi ya kujishindia baiskeli na pikipiki," alisema.

# TARI Ilonga sasa yaanza kuzalisha mbegu kisasa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kupitia kituo cha Ilonga, wilayani Kilosa mkoani Morogoro, imeanza kuzalisha mbegu za kisasa za alizeti ili kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi wa uzalishaji wa mbegu hizo, Mratibu wa mradi huo, Frank Reuben alisema umelenga kuipunguzia serikali mzigo wa kutumia fedha nyingi kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi.

Alisema unaendeshwa na TARI na kufadhiliwa kwa pamoja kati ya serikali na taasisi ya kuboresha mifumo ya masoko ya kilimo nchini (AMDT), umeingia mikataba na kampuni tatu za uzalishaji wa mbegu za alizeti ambazo zitawatumia wakulima, ili kuzalisha mbegu hizo.

Mratibu huyo alisema kuwa mbegu hizo zitazalishwa na kampuni za kutoka Nyanda za Juu Kusini, Mikoa ya Kanda ya Mashariki na Mikoa ya Kanda ya Kati na kisha kusambazwa kwa wakulima wa maeneo hayo kwa ajili ya kilimo cha alizeti, hatua ambayo itasaidia kusindika mafuta ya kula na kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji.

"Ili tuweze kujitosheleza kwa mafuta ya kula tunahitaji tani 13,000 zao la alizeti pekee na hili linawezekana kupitia mikakati kama hii ya uzalishaji wa mbegu bora za alizeti pamoja na zao la michikichi na yote ikasindikwa mafuta," alisema Mtafiti Reuben.

Naye, Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti TARI Ilonga, Dk. Lameck Makoye, alisema nje ya mradi huo tayari wametayarisha mashamba kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu hizo fedha ambazo zinagharimiwa na serikali.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa wazalishaji wa zao la alizeti nchini, Stephen Marealle, alipongeza serikali kuja na mradi huo wa kutatua changamoto ya mafuta nchini na kushauri kuchukua hatua za haraka za ujenzi wa maghala ya kuhifadhi na kusambaza mbegu za zao hilo, ili kuwafikia wakulima wengi zaidi nchini.

Alisema ukosefu wa maghala ya kuhifadhia zao hilo huwalazimu kipindi cha mavuno kuuza kwa bei ya kutupa badala ya kuhifadhi kama mazao mengine ya mahindi na mpunga.

Aidha, Mkurugenzi wa Taasisi ya AMDT ambao wamefadhili mradi huo, Charles Ogutu, alipongeza Serikali ya Tanzania kwa juhudi wanazofanya za kuhakikisha wanamaliza tatizo la upungufu wa mafuta ya kula nchini na wapo tayari kushirikina nao.

# Wananchi wakumbushwa chanjo ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wametakiwa kutofanyia mzaha suala la kupata chanjo ya UVIKO-19, badala yake wajitokeze kwa wingi katika vituo vya kutolea huduma hiyo ili kujikinga na ugonjwa huo.

Aidha, wamekumbushwa UVIKO-19 ni janga la dunia, na kwamba mtu ambaye anasita kupata huduma hiyo hawezi kuruhusiwa kuingia nchi nyingine kama atakuwa hajachanjwa.

Wito huo jana umetolewa na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya alipokuwa akitoa salama za Pasaka za taasisi hiyo kwa Watanzania.

"Dunia inasumbuliwa na ugonjwa huu, nasi kama taasisi tunaona ni muhimu kukumbusha Watanzania kwamba wasiufanyie mzaha, badala yake kila mmoja aende katika kituo achanjwe," alisema Ngawaiya.

Alisema, Dar es Salaam ni miongoni mwa mikoa ambayo iko nyuma kwenye suala la chanjo ambapo amewataka wakazi waache ubishi kwenye jambo la msingi kama chanjo ya UVIKO-19.

Mwenyekiti huyo alisema, hivi karibuni alimsikia Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Rashid Mfaume akitoa takwimu za watu waliochanja mkoani humo kuwa ni 571,712 tu. "Dk.Mfaume alionyesha kushangazwa kasi ndogo ya watu waliojitokeza kuchanja na kutaka kasi iongezeke, nasi CEGODETA tunasisitiza hilo kuwa suala la kupata chanjo ni la muhimu," alisema.

Alisema, anatambua jinsi wakazi wa mkoa huo walivyo na shughuli nyingi, lakini akasisitiza kuwa ni vyema watu wazifanye huku wakiwa tayari wana chanjo vinginevyo wanaweza kushindwa kuendelea na shughuli hizo.

"Niwakumbushe kuwa ujanja ni kuchanja si kukwepa, kwani wale wanaokwepo, kuna sehemu watakwama tu, hivyo katika salamu zetu za Pasaka, tunasisitiza Watanzania kuchanja," alisema.

Mwenyekiti huyo pia alizungumzia suala la Anwani ya Makazi na kuipongeza serikali kwa kuanzisha mfumo huo kwa kuwa unajumuisha taarifa za kijiografia, wamiliki na wategemezi wa Anwani.

"Yapo mengi katika mfumo huo na faida zake ikiwamo kila mtu anayeishi Tanzania kuwa na anwani halisi ya makazi, kila biashara inayosajiliwa Tanzania itakuwa na anwani halisi ya makazi,"alisema.

Aliongeza kuwa utambulisho wa watu wanaoishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utarahisisha usajili wa mali, biashara, vizazi na vifo utaboreshwa na kwamba huduma za dharura, zikiwamo za polisi, zimamoto na magari ya wagonjwa, zinaweza kutambua maeneo yenye dharura na kuyafikia kirahisi.

"Lakini pia wageni wanaweza kubaini mahali wanakokwenda kirahisi, benki na taasisi nyingine za fedha zitaboresha utendaji kazi wao, mamlaka za mapato zitabaini walipa kodi kirahisi," alisema.

Alisema, CEGODETA inaamini kuwa kampuni zinazotoa huduma kwa umma zitaboresha huduma zake na kwamba muda mfupi utatumika katika utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi ikiwamo usafiri na huduma za posta.



Mmoja wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akiuliza swali wakati wa kongamano la Wanafunzi la AISEC lililofanyika chuoni hapo chini ya udhamini mkuu wa kampuni ya Barrick. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi wa maji washika kasi

**Na Joseph Mwendapole**

MRADI wa maji Kigamboni - Kimbiji mkoani Dar es Salaam unaendelea kushika kasi ambapo inaelezwa kuwa kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kwenda kwa wananchi imeanza kwa ufanisi.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na msimamizi wa mradi, Mhandisi Farida Kyamani, wakati akielezea utekelezaji wa mradi huo unaofanywa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) .

Alisema kazi ya kuchimba na kulaza bomba kubwa la inchi 16 ilianza wiki iliyopita na sasa kazi inaenda kwa kasi ili kuhakikisha inakamilika ndani ya muda uliopangwa.

Alisema kuwa kazi inayofanyika ni kuchimba na kulaza bomba kwa umbali wa kilomita 7 kutoka kwenye kata ya Kibada mpaka Mjimwema kwa Mwingira.

"Kwa sasa kazi inaendelea kwenye eneo la Kibada - Mwasonga ya kulaza bomba la inchi 16, kazi hii itasaidia kutoa huduma ya majisafi kwenye kata mbalimbali ikiwemo kata ya Somangila, Mjimwema, Kisarawe II, Kibada, Vijibweni na Tumbi," alisema

Mhandisi huyo alisema wananchi watapata majisafi kutoka kwenye tenki kubwa la lita milioni 15 ambalo ni sehemu ya mradi huo.

Mradi wa maji Kigamboni - Kimbiji unatekelezwa na DAWASAkwa gharama ya Sh bilioni 25, ukihusisha ujenzi wa visima saba vya kuzalisha maji kwenda kwenye tenki.

# Viongozi wa Ruangwa kuwezeshwa mafunzo

**Na Sabato Kasika**

VIONGOZI wa ngazi mbalimbali katika Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, wanatarajia kupata mafunzo yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu, kupitia mradi uitwao 'Kukuza Uwazi na Uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa' (MSM).

Mradi huo uliozinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wiki iliyopita, unatekelezwa na Jukwaa la Elimu ya Uraia Tanzania Civic Education in Tanzania (CETA).

Mratibu na mwezeshaji wa mradi huo, Uzima Justine, aliiambia gazeti hili juzi kuwa, wataanza kutoa mafunzo hayo mwezi ujao hadi Agosti mwaka huu, katika tarafa tatu kata 22 vijiji 90 na vitongoji 436 wilayani humo.



Ukurasa 12

Ulipo Twaja; staili mpya Takukuru inapeleka shule penye mikusanyiko


Ukurasa 13

Kukosa mlo mchana kunavyoshusha ufanisi elimu shule mkoa Shinyanga

Nipashe

# TESA

Jumanne Aprili 19, 2022

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Watendaji wa Ruangwa wapelekewa darasa maalum la kuwajibikia kazi

## • Ngazi mitaa hadi kata kunolewa upya

WIKI iliyopita, wakazi wa mji wa Ruangwa mkoani Lindi walishuhudia uzinduzi wa mradi wa mafunzo kwa viongozi utakaowawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu katika jamii wanayoiongoza.

Hatua hizo zinachukuliwa kutokana na kile kinachoelezwa kuwa kuwapo kwa changamoto nyingi zinazosababisha msuguano kati ya viongozi kuanzia ngazi ya vijiji hadi wilaya katika maeneo mbalimbali nchini.

Ruangwa ni miongoni mwa wilaya zenye changamoto hiyo ambako mradi uitwao Kukuza Uwazi na Uwajibikaji Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa' (MSM) umefika ili kuwaonoa viongozi.

Mwaka jana mradi kama huo ulifanyika wilayani Urambo mkoani Tabora sasa umetua Ruangwa ili kusaidia viongozi wakiwamo watendaji wa kata kutimiza majukumu yao inavyotakiwa.



Viongozi mbalimbali wa Wilaya ya Ruangwa, kwenye ufunguzi wa mafunzo ya utawala bora, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MATADAO**

Mratibu na Mwezeshaji wa mradi huo Uzima Justine, anasema sababu kuu ya mradi huo kupelekwa Ruangwa, ni kwamba watendaji wengi kwa sasa hawapati mafunzo ya uongozi, hali inayosababisha migogoro kati yao na wananchi.

"Kwa mfano watendaji wengi ni wale waliohitimu vyuo vikuu hajasomea mambo ya serikali za mitaa, hivyo ni wazi utendaji wao unaweza kuwa na changamoto nyingi," anasema Justine.

Anafafanua kuwa yapo makosa mengi ya kisheria na kiuongozi ambayo wamekuwa wakiyafanya kwa kutojua, na kwamba ni muhimu waelimishwe ili wafanye kazi yao kwa weledi.

"Wakati tunazindua mradi huu Ruangwa, Mheshimiwa Nape Nnauye naye ameomba twende jimboni kwake Mtama, hivyo tukiwa na fungu mwaka ujao, tutakuwa Mtama kwani hili ni tatizo la nchi nzima," anasema.

### AINA YA ELIMU

Ni mafunzo maalum kwa viongozi wilayani Ruangwa mkoni Lindi ambayo yataanza kutolewa kwa lengo la kufanya kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria za nchi, kanuni, miongozo na taratibu za serikali za mitaa.

Elimu inayotajwa kupitia mradi wa Kukuza Uwazi na Uwajibikaji Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) ambao unatekelezwa na Jukwaa la Elimu ya Uraia Tanzania Civic Education in Tanzania (CETA).

Mratibu na Mwezeshaji wa mradi huo Uzima Justine, anasema utaanza kutekelezwa mwezi ujao hadi Agosti mwaka huu, katika tarafa tatu, kata 22, vijiji 90 na vitongoji 436 wilayani humo.

Justine anasema, mradi huo wa mwaka umefadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Ujerumani la Hanns Seidel Foundation (HSF) la Jijini Dar es Salaam unatoa mafunzo ya kimkakati ya utawala bora kwa wenyekiti na watendaji wa vijiji 90, kata 22, maofisa maendeleo ya jamii wa kata, madiwani wote 29 wa halmashauri ya wilaya hiyo watanufaika.

Anasema, hivi karibuni kila ngazi itakuwa na tarehe yake ya mafunzo, na kwamba washiriki wataitwa katika ukumbi na kufundishwa na wataalam walioandaliwa na mradi huo.

"Baada ya mafunzo hayo, kuanzia Septemba hadi Desemba kutakuwa na tathmini pamoja na kukazia mafunzo, kwani kutakuwa na ufuatiliaji ili kupima matokeo ya mafunzo hayo na ufuatiliaji huo utaambatana na kufundisha zaidi pale ambapo hapakueleweka vizuri darasani," anasema.

"Anasema, viongozi watasaidiwa kuelewa kwa vitendo, lengo la mafunzo hayo ili hatimaye watimize wajibu wao kwa kuzingatia taratibu na miongozo inayotakiwa katika uongozi wanapotumikia wananchi.

Karl-Peter Schonfisch kutoka HSF,anasema wamekubali kufadhili mradi huo kwa imani kwamba, wananchi wataongozwa na viongozi wanaoelewa majukumu yao, kwa kuwa watakuwa wamepikwa na kuiva.

### MWENYEKITI RUANGWA

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Andrew Chikongwe, alisema mradi huo ni wa kihistoria kwa wilayani mwake kwa kuwa haijawahi kutokea mradi kuhusisha idadi kubwa ya viongozi kwa mafunzo ya pamoja.

Anasema, matumaini yake ni kwamba mwisho wa mradi yeye na wenzake watakuwa viongozi wapya, kwa kuwa watakuwa wamenolewa vya kutosha jinsi ya kutumikia wananchi.

"Ni mshangao, kwani haijawahi kutokea katika wilaya yetu kuona mradi kama huu wa kuhusisha idadi kubwa ya viongozi kwa mafunzo ya pamoja, ila ninaamini kuwa tutapata faida kubwa," anasema Chikongwe.

Anasema, ni muhimu wenyeviti na watendaji wa serikali ngazi za vijiji na kata wilayani humo kutumia fursa ya kushiriki kikamilifu mafunzo yao utawala bora ili kuongeza uelewa na hatimaye kutimiza wajibu wao inavyotakiwa.

ELIMU
NA RENATHA
MSUNGU, DODOMA

# Ulipo Twaja; staili mpya Takukuru inapeleka shule penye mikusanyiko

## • Yawavamia, darasa papo kwa hapo



Wafanyabiashara wa samaki katika Soko la Bonanza lililopo jijini Dodoma, wakimsikiliza Ofisa Uelimishaji kutoka Takukuru mkoani Dodoma (hayupo pichani). **PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma kwa miezi mitatu imekuwa ikiendesha kampeni iliyobuni na kuipa jina 'Ulipo Twaja' nia yake kuelimisha wananchi madhara ya kutoa na kupokea rushwa kazini, pasipo kuathiri shughuli zao za kimaendeleo.

Ni kampeni iliyoendeshwa miezi mitatu mkoani Dodoma, kati ya Januari 18,2022 na kukoma tarehe 31 mwezi uliopita, nia ni kuwafikia wakazi waliolengwa jijini hapo kwa mafanikio ya asilimia 86, ikitoa elimu namna ya kuzuia na kupambana na rushwa kwa wakazi waliopo katika mikusanyiko ya shughuli zinazokuza uchumi.

Mkuu wa Takukuru mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo anasema, 'Ulipo Twaja' ni kampeni ambayo maofisa uelimishaji wa Takukuru wanazuru penye mikusanyiko ya watu kama vile vijiwe vya bodaboda, sokoni, mnadani na mikutano ya hadhara, lengo kuelimisha namna ya kujikinga.

Anasema wameamua kutumia mbadala huo, baada ya kubaini wengi wanashindwa kuhudhuria mikutano ya kutoa elimu wanayoiandaa Takukuru, kupata njia sahihi ya kinga, pia kuzuia rushwa, hivyo wanaamua kuwaelimisha, huku wenyewe wakiendelea na shughuli zao za kawaida

Kwa mujibu wa Kibwengo, Takukuru imebuni utekelezaji wa kampeni hiyo, kwa sababu wanaamini suala la kupambana na rushwa si la taasisi hiyo pekee, bali kila mtu anapaswa kuwajibika na uzuiaji rushwa popote alipo.

Anafafanua mantiki ya mkakati huo, kwamba ni njia ya kukuza hamasa ya wananchi kushiriki uzuiaji rushwa, ikiwamo kuwaongezea uelewa na utambuzi wa dhana 'rushwa ni adui wa haki katika maendeleo', hivyo wanapaswa kuipinga.

Kibwengo anasema hakuna gharama yoyote kwa wananchi kushiriki mapambano dhidi ya rushwa, hivyo ni vyema anastahili kutoa ushirikiano kwa elimu hiyo kutoka Takukuru, hata ukajengeka utamaduni wa kupambana na rushwa.

Hivyo, anaiasa sasa ijiamini kwani mapambano dhidi ya rushwa daima si jukumu la serikali pekee, bali kila mmoja anawajibika kuwa mlinzi wa mwenzake katika mapambano dhidi ya rushwa.

Anaeleza mkazo mkubwa wa kazi hiyo ni kukuza ufahamu, utayari na uthubutu wa kuwa majemedari wa mapambano kukabili rushwa, wakibadili mtazamo wa maovu yanayoakisi nyoyo za baadhi ya wenye dhamana ya kusimamia rasilimali za umma.

Mkuu huyo wa Takukuru mkoa, anafafanua mantiki na mbinu iliyoko ni kwamba, suala la kubadili mtizamo hasi dhidi ya jambo lolote, linahitaji elimu kuwafikia wengi kutoka rika na makundi mbalimbali, ili nao wakasambaze elimu kwingineko.

Anasema 'Ulipo Twaja' inagusa mikusanyiko ya wananchi, pasipo kujali muda kuanzia asubuhi hadi jioni, kutegemea na muda na aina ya mkusanyiko wa waelimishaji husika.

Anaeleza namna kampeni ilivyochukua nafasi ni wakati wahusika wakiendelea na shughuli zao za kila siku katika maeneo yao ya kazi.

### MATARAJIO YA TAKUKURU

Kibwengo anasema matarajio yao ni kwamba, baada ya elimu na ushawishi wa macho, masikio, kusoma vipeperushi yatakoleza chachu ya mabadiliko ya kutofumbia macho rushwa, kwa kushirikiana na serikali.

Pia, anataja imani yake kwamba itawachagiza wananchi kushirikiana na serikali kuzuia vitendo vya rushwa visitokee, hata wakaondokana na dhana ya kukaa kando wakabaki watazamaji, pasipo kuchukua hatua kukabili wanaojihusisha na ubadhirifu wa haki kupitia rushwa.

Kibwengo anaeleza imani yao kwamba, askari wa awali katika kuzuia rushwa ni mwananchi mahali alipo kwa njia ya kubadili mtizamo hasi, wakitumia nyenzo sheria, kanuni na taratibu zilizopo za kuheshimu haki na usawa, wakitambua na kuthamini maadili na misingi ya uzalendo.

> 'Ulipo Twaja' inagusa mikusanyiko ya wananchi, pasipo kujali muda kuanzia asubuhi hadi jioni, kutegemea na muda na aina ya mkusanyiko wa waelimishaji husika.



Mkuu wa Takukuru mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, akizungumza na wanafunzi (hawapo pichani) kuhusu umuhimu wa elimu ya kupinga rushwa.

### HALI ILIVYO

Kibwengo anasema, idadi ya taarifa ambazo Takukuru inazipokea kwa njia ya simu kuhusu rushwa na ukiukwaji wa maadili, imeongezeka sana katika kipindi cha kampeni, ikiwa ni kiashiria kampeni imefanikiwa.

Anasema Takukuru Mkoa wa Dodoma, inaamini kupanda mbegu ya mabadiliko kwenye mioyo ya wakazi wake, ni namna ya kuwafanya watimize wajibu wao kwa kuzuia vitendo vya rushwa, kabla ya hata kuwasiliana na Takukuru.

Kibwengo anajigamba'Ulipo Twaja imepandwa na daima haitakufa bali inapaswa ikue na kuwa mti mkubwa wenye mizizi mikubwa isiyoyumbishwa.

### WATUMISHI, WAPOKEAJI

Sabeth Mshana ni mwelimishaji, anayesema mwitikio umeonekana kuwa juu ,kutokana na kampeni hiyo kuwafuata wananchi waliko kwenye mikusanyiko inayowahusu wakiendelea na shughuli zao kimaendeleo.

Mshana anasema, wamekuwa wakitumia nyenzo kama vipaza sauti na kuainisha namna ya jamii inaweza kuwaeleza madhara yatokanayo na kupokea au kutoa rushwa.

Anasema mbali na sokoni pia vijiwe vya bodaboda, pia kuna vituo vya kutoa huduma za afya, penye shughuli za uvuvi ambako walionekana kuifuatilia kwa karibu, wakiguswa hata wakidadisi kwa maswali mengi kutaka kuelewa kwa kina uzuiaji na kutoa rushwa.

Faustine Malecha, Ofisa Uelimishaji kutoka Takukuru, anayewataka wafanyabiashara kuwa wazi wanapohitaji kupata stahiki zao kutoka kwa viongozi wa soko na kwingine wanakofanya biashara na wasikubali kutoa rushwa.

Anawaelemisha kwamba wasikubali kupita njia zisizo halali, kwa sababu zitawapa shida baadaye watakapogundulika kutoa rushwa

Martha Martine, ni mjasiriamali anayeishukuru Takukuru kwa kuwafikia waliko kwenye mikusanyiko, ambako kumewasaidia kwa kiasi kikubwa kupata uelewa namna ya kujikinga na rushwa katika maeneo yao ya kazi.

Anafafanua kwamba, hivi sasa wanajua kuzitafuta haki zao popote waliko, kwa sababu wanayo elimu ya kujikinga na rushwa inayotolewana Takukuru katika maeneo mbalimbali.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Kukosa mlo mchana kunavyoshusha ufanisi elimu shule mkoa Shinyanga

• Wenyewe wakiri wanasinzia darasani
• Matokeo mabaya msingi na sekondari

INAANGUKIA msamiati 'shida juu ya shida'. Wanafunzi walioko vijijini mkoani hapa, wamekuwa wakisoma umbali mrefu hasa baadhi kufika kati ya kilomita 10 hadi 20, wanapoenda na kurudi masomoni na hasa, kata inapokuwa na sekondari moja.

Hiyo ni moja, watoto hao pia wanakabiliwa na kushinda njaa kutwa nzima, vyote matokeo yake wanashindwa kufanya vizuri kitaaluma.

Shule ya Sekondari Pandagichiza wilayani Shinyanga, imo katika zinazowakilisha shule nyingi zinazobeba dhamana ya viashiria husika, wanafunzi wake wanatoka umbali mrefu, hata wanafanya vibaya kitaaluma, kukiwapo malalamiko wanashinda na njaa.

Ofisa Elimu wa Kata ya Pandagichiza, wilayani Shinyanga, Irene Edward, anasema wameanzisha mkakati wa kutoa chakula kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, ambao wapo kwenye madarasa ya mitihani.

Anasema ni uamuzi uliofikiwa kutokana na kuwapo wanafunzi watokao mbali, wanashinda njaa, hata imeathiri matokeo ya mtihani darasa la saba na kidato cha nne.

"Mwanafunzi anapokaa shuleni muda mrefu bila kula chakula, hawezi hata kuelewa masomo sababu ya kusumbuliwa na njaa, atakuwa akisinzia tu darasani," anasema Edward.

Anaendelea: "Mkakati uliopo kwa sasa ni kutoa kipaumbele kwa kutoa chakula kwa wanafunzi ambao wapo kwenye madarasa ya mtihani kuanzia darasa la nne na saba, kwa sekondari kidato cha pili na nne. ambapo tutahamasisha wazazi wachange, pamoja na kutumia chakula cha mashamba ya shule."

Diwani wa Pandagichiza, Charles Kabogo, anasema ulaji chakula kwa wanafunzi shuleni ni chachu ya kukuza taaluma, akiwataka wazazi katika kipindi cha mavuno, watenge chakula cha kuchangia shuleni kwa watoto wao kiwaletee mageuzi ya kitaaluma.

"Matokeo ya mtihani wa darasa la saba na kidato cha nne uliofanyika mwaka jana, shule zetu za hapa Pandagichiza zilifanya vibaya sana, matokeo ambayo sikufurahishwa nayo, tumeshuka sana kitaaluma,"anasema Diwani Kabogo.

## WALIMU WAANIKA

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Pandagichiza Laurent Richard, anasema kuna wakati wanafunzi walipokuwa wakinywa uji shuleni, walikuwa wakifanya vizuri masomoni, lakini baada ya chakula cha shule kuisha wakasitisha huduma hiyo, ndipo wakaanza kufanya vibaya kitaaluma.

Anasema, wameweka mikakati ya wanafunzi waliopo darasa la nne na saba sasa, waanze kula shuleni, kuwasaidia kuendana na masomo.

"Chakula ni muhimu sana kwa wanafunzi shuleni, mfano kabla ya chakula cha shule kuisha huwa tunalima kwenye mashamba ya shule na tulikuwa tukipika uji angalau wanafunzi wapoze njaa. Walikuwa wakielewa sana masomo yao, lakini baada ya kusitisha kutoa uji hali ikawa tofauti,"anasema Mwalimu Mkuu Richard.

"Matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba ambao ulifanyika mwaka jana, walifanya wanafunzi 50, waliofaulu 23 na walifeli 27, matokeo ambayo ni mabaya na hii inatokana na wanafunzi kutokula chakula shuleni, wengine kutoroka vipindi kwenda kula nyumbani kwao na wakienda hawarudi sababu ni mbali, "anafafanua.

Mwalimu wa Afya na Chakula wa Shule ya Msingi Pandagichiza, Lucia Maungo, anaeleza mwanafunzi anapokaa muda mrefu shuleni bila ya kupata chakula, afya yake kiakili haikai sawa na hata mwili wake unadhoofika.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Pandagichiza, George Vangilisasi, anasema shule inalima chakula kwenye mashamba yake na mwaka juzi msimu wa kilimo uliopita walipata magunia 10 ya mahindi, ndiyo waliyatumia kulisha wanafunzi.

"Shule yetu hii ya Sekondari Pandagichiza baada ya chakula magunia 10 kuisha na kusitisha huduma ya utoaji chakula, matokeo ya mtihani kidato cha nne uliofanyika mwaka jana tulifanya vibaya sana, ndipo tukagundua kumbe ili tupate matokeo mazuri lazima wanafunzi wapate chakula," anasema Vangilisasi.

"Matokeo yetu ya kidato cha nne mwaka jana (2021), wanafunzi waliopata daraja la kwanza walikuwa wawili, daraja la pili 6; la tatu 18, la nne 68, na waliopata ziro 34,"anafafanua.

Anasema kwa mkakati waliokubaliana na uongozi wa kata ni kuhamasisha wananchi kuchangia chakula wakati wakisubiri mavuno ya shamba lao la shule, ili waanze kuwapatia chakula wanafunzi walioko kwenye madarasa ya mtihani, kidato cha pili na nne.

> "Suala la kuchanga chakula halina shida, isipokuwa kwa sasa hawana chakula na wanategemea hadi msimu wa mavuno.

## WANAFUNZI WAFUNGUKA

Mwanafunzi Felista Jilala, anayesoma darasa la saba katika Shule ya Msingi Pandagichiza, anasema kuwa vipindi vya asubuhi huwa wanavielewa, lakini ikifika mchana huwa wanasikia njaa hata kushindwa kuzingatia masomo.

Anasisitiza suala la chakula shuleni ni muhimu sana kwa sababu awali walipokuwa wakinywa walau uji uliwasaidia kuelewa masomo, lakini baada ya kuacha hali ikawa tofauti na kuna wakati baadhi ya wenzao wanatoroka kukwepa kushinda njaa.

Mwanafunzi Paschal Mwambila, anayesoma kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Pandagichiza, anasema kukiwapo ukosefu wa chakula shuleni, kamwe mwanafunzi hawezi kuzingatia masomo yake kwa sababu ya kusumbuliwa na njaa, rai yake ni walau wapatiwe hata uji kupunguza makali ya njaa.

"Njaa ni mbaya sana tena ikikukamata vizuri unaishiwa hadi nguvu. Tunaiomba tu serikali ihamasishe ulaji chakula shuleni hasa katika shule za vijijini na kusisitiza wazazi kuchangia angalau tuwe tunakunywa hata uji kama zamani, kwa sababu kuna wanafunzi wengine wanatoka mbali," anasema Mwambila.

Maria Kashinje, wa kidato cha tatu shuleni Pandagichiza, anatoa undani wa simulizi ya mikasa ya kukosekana mlo shule, unavyomrahisishia mwanafunzi hata akiambiwa na mzazi asiende shule kwa mbadala akalime, inakuwa rahisi kukubali na ndio utoro shuleni unapoanzia, akihofu kushinda na njaa masomoni.

Mzazi Martha George, anasema wao suala la kuchanga chakula halina shida, isipokuwa kwa sasa hawana chakula na wanategemea hadi msimu wa mavuno.

Anakiri ukweli namna watoto wao wanavyopata shida ya kusoma wakiwa na njaa shuleni, huku wakitembea umbali mrefu, hasa kwa waliopo sekondari.

Martha analalama kwamba, kwa kipindi kilichopo cha mvua hawana akiba ya chakula na wanategemea kupata chakula kwenye msimu wa mavuno miezi kadhaa ijayo.

INAENDELEA UK.14



Wanafunzi wakichukua chakula shuleni. **PICHA: MTANDAO**

# Kukosa mlo mchana kunavyoshusha ufanisi elimu shule mkoa Shinyanga

INATOKA UK.13

**VIONGOZI WA SERIKALI**

Mwenyekiti wa kijiji cha Pandagichiza, James Sitta, anasema katika kipindi cha mavuno, wataitisha mkutano wa hadhara, na kuhamasisha wananchi kuchangia chakula shuleni kwa shule zote za msingi na sekondari, ili wanafunzi wake waanze kupata chakula, hata kuwawezesha kufanya vizuri kitaaluma.

Anaungwa mkono na Mwenyekiti wa Kijiji cha Shilabela, Emmanuel Magadula, anayesema kwa sasa wazazi hawana chakula cha kuchanga, lakini kipindi cha mavuno itakuwa rahisi. Kwa sababu watakuwa na akiba nyingi ya chakula.

Ofisa Kilimo wa Pandagichiza wilayani Shinyanga, Sylivanus Homera, anasema hali ya chakula msimu wa kilimo uliopita (2020-2021) ilikuwa nzuri, pamoja na kupata chakula kingi kwenye mashamba ya shule, hali ambayo wanafunzi walikuwa wakila chakula pamoja na kunywa uji.

Anasema mfano katika Shule ya Msingi Ng'wamadelahna, ambapo walikuwa na shamba darasa, walipata maguni 28 ya mahidi ambayo yalikuwa yakitumiwa na wanafunzi kupata chakula.



Wanafunzi wakishiriki mlo wa shule, ambayo ni muhimu kwa afya yao ya akili. **PICHA: MTANDAO**

"Msimu wa kilimo uliopita (2020-2021) ulikuwa mzuri, ambapo kulikuwa na chakula kingi, lakini msimu wa mwaka (2021-2022) hali haitabiriki ambapo mwanzoni kulikuwa na ukame sana, na hivyo wananchi kuchelewa kulima ambapo tuna hofu huenda kusiwe na chakula kingi kama msimu uliopita," anasema Homera.

Ofisa Lishe Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Said Mankiligo, anasema hali ya lishe wilayani humo siyo nzuri, watoto asilimia 33.2 wana udumavu na kubainisha mikakati iliyopo ni kutumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii kuhamisha wananchi kuwapatia watoto wao lishe bora, pamoja na utoaji chakula mashuleni.

Ofisa Lishe Mkoa wa Shinyanga, Denis Madeleke anasema kati ya watoto 100 mkoani humo 32 wanakabiliwa na tatizo la udumavu, pamoja na asilimia 59 kukabiliwa na tatizo la upungufu wa damu, na kusema utoaji wa chakula shuleni utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo hilo la udumavu na upungufu wa damu.

"Naunga mkono suala la utoaji wa chakula shuleni, hasa kwa shule za maeneo ya vijijini ni muhimu sana katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa damu kwa watoto na kuimarisha afya zao, sababu uzingatiaji ratiba za lishe ni muhimu sana katika makuzi ya mtoto na ukomavu wake kiakili," anasema Madeleke.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Sophia Mjema, anasema ukosefu wa lishe bora kwa watoto ni tatizo, hata shuleni hawataelewa vizuri masomo yao, na hata hapo baadae taifa kuja kukosa wataalamu wake wa kuliendeleza.

Anawaagiza Maofisa lishe kwa kushirikiana na wahudumu wa Afya ngazi ya jamii, watoe elimu kwa wananchi kuzingatia masuala ya lishe bora kwa watoto wao, ili wawe na afya njema na hata wanapokuwa darasani wafanye vizuri masomo yao, na kusema kuwa suala la utoaji chakula shuleni ni makubaliano ya wazazi wenyewe.

## WANENAVYO MALENGA

### NANENEPESHA KIBUBU

• Kama siyo njaa yangu, ningekivunja kikombe,
Huo ndio moyo wangu, nioneni ni mzembe,
Ninatoa jasho langu, mali kwangu ndio jembe,
Nanenepesha kibubu, nikitemwa nisiyumbe.

• Kikombe hiki si changu, sikinywei hata chembe, Hakipendwi huku kwangu, kinakata kama wembe,
Nawambia ndugu zangu, msinifanye niyumbe,
Nanenepesha kibubu, nikitemwa nisiyumbe.

• Kula muhogo mchungu, kwangu mimi ni kimbembe,
Nainama kwa uvungu, japo niipate sembe,
Hii ndiyo hali yangu, kwayo ninashinda kombe,
Nanenepesha kibubu, nikitemwa nisiyumbe.

• Hii siyo kazi yangu, ndio nakupa ujumbe,
Usijenipiga rungu, nikaupata uvimbe,
Mimi nashiba kivyangu, acha kafiri atambe,
Nanenepesha kibubu, nikitemwa nisiyumbe.

• Ingekuwa kazi yangu, mngeniacha niimbe,
Nimsifu Mungu wangu, na shetani nimchambe,
Hapa dinari ni yangu, siiachi hata chembe.
Nanenepeha kibubu, nikitemwa nisiyumbe.

• Nakwambia ndugu yangu, kutemwa usikuombe,
Kukumeza ni kuchungu, utazitafuta tembe,
Tuzidi muomba Mungu, kazi zitupe maembe.
Nanenepesha kibubu, nikitemwa nisiyumbe.

• Kwa huyu tajiri wangu, hana shida hata chembe,
Nikifanya kazi zangu, anisifu mi kiumbe,
Napata bonasi yangu, sasa ninajenga Kwembe,
Nanenepesha kibubu, nikitemwa nisiyumba.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### HABARI HIZI ZATISHA

Habari hizi zatisha, tena zinasitikisha,
Daktari katupasha, bila ya kutuzungusha,
Mimba mnaporomosha, uhai kuukausha,
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

Si wote nawavumisha, wale mimba wanashusha,
Ni wale wawafikisha, sipitali kujikosha,
Wakati wameshashusha, hali mbaya zawatisha,
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

Dokta kafahamisha, wale wanawafikisha,
Hoi hali zinatisha, mimba wakizidondosha,
Nusu walazwa watosha, mimba zinawaendesha,
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

Tena chakusikitisha, mimba mnavyozishusha,
Njia zenu mwakatisha, badaye mwahangaisha,
Sipitali wafikisha, kwa tiba inayotosha,
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

Wanaowasababisha, eti mwawaunganisha,
Mliokula maisha, kulea wajikausha,
Vipi kuanza maisha, bila ya kujiridhisha?
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

Dokta kafahamisha, umri mmefupisha,
Miaka kujumlisha, kumi na tano yatosha,
Bila ya kuizidisha shinatano mnatisha!
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

Hatari mwakaribisha, katika yenu maisha,
Utasa kukaribisha, na magonjwa ya kutisha,
Saratani kuwafisha, ni maandalizi tosha,
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

Na tena inaonesha, kinga mmedhoofisha,
Mnazidi kukiwasha, na mimba wanatungisha,
Virusi ukimwi hasha, hamjali mwakausha,
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

Mbeya mnaivumisha, vibaya yenu maisha,
Tena mwaiwakilisha, kwa mambo yanayotisha,
Hapo mmejiangusha, mbele nenda badilisha,
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

Wasichana nakumbusha, maua yamechavusha,
Kama mwajirahisisha, ni jamvi mwatuketisha,
Na mkijihadharisha, mtafaidi maisha,
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

Wenye dini nakumbusha, haramu watoto fisha,
Mjue mwajifikisha, pabaya yale maisha,
Mungu akiliamsha, mateso hatakatisha,
Wasichana huko Mbeya, tabia yenu si nzuri.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Wananchi washukuru kupatiwa fedha ujenzi wa shule

**Na Renatha Msungu,** BAHI

WANANCHI wa Kata ya Mpinga, wilayani Bahi, mkoani Dodoma wameishukuru serikali kwa kuwapatia zaidi ya Sh. milioni 700 kwa ajili ya ujenzi wa shule za msingi na sekondari ambazo zimesaidia kupunguza kero ya watoto kutembea kilometa saba kufuata shule ilipo.

Aidha, wamemuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwajengea barabara ambazo zitafungua mawasiliano ya kibiashara na uchumi kati yao na kata jirani za Kigwe na Nala.

Akizungumza na Nipashe kijijini hapo, Simon Omary, alisema kujengwa kwa shule hizo kutasaidia kuongeza mahudhurio kwa wanafunzi ambao wengine walikuwa watoro kutokana na kutembea umbali mrefu.

Alisema serikali imekumbuka kuwajengea shule nyingine ambazo zitapunguza idadi kubwa ya wanafunzi wanasongamana kwenye darasa moja na kuwafanya watoto kushindwa kusoma vizuri.

Naye, Diwani wa kata hiyo, Kudagana Ndallu, alisema serikali imewapa Sh. milioni 120 ambazo walizitumia kujenga vyumba sita vya madarasa ya shule ya msingi shikizi katika vijiji vya Mpinga na Mzogole na alihamasisha wananchi wakajitolea kujenga madarasa mengine mawili kwa Sh. milioni 40 kufikisha madarasa nane.

Alisema baada ya ujenzi huo serikali ikatoa Sh. milioni 600 ambazo wanazitumia kujenga shule ya sekondari yenye vyumba nane vya madarasa.

"Naishukuru serikali kwa kuamua kwa dhati kuondoa tatizo la ukosefu wa sekondari katika Kata ya Mpinga," alisema.

Kwa upande wake, Mratibu Elimu wa kata hiyo, Hamis Nalianga, alisema kuwa awali wanafunzi wa kata hiyo walikuwa wakitembea kwenda kata jirani ya Kigwe umbali wa zaidi ya kilometa saba kusoma.

"Kweli tulipokea fedha toka halmashauri ya wilaya yetu ya Bahi kwa ajili ya kujenga shule iliyokamilika ya sekondari ambayo ina jengo la utawala, chumba cha kompyuta, maabara, vyumba nane vya madarasa, vyoo vya wanafunzi vyenye matundu 20 na vya walimu," alisema.

Aliwataka wazazi na wananchi wa kata hiyo kulindana, kuitunza shule hiyo kwa kuwa ni mali yao pamoja na kuwa serikali ndiyo iliyoijenga.

"Tunatarajia kumaliza ujenzi katikati ya mwaka huu na kukabidhiwa kwa wananchi wa kata hii, hivyo nitoe wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha wanaitunza pamoja na shule hizo shikizi kwa kulima majani kwa kutoingilia mipaka ya shule," alisema.

# Kada ya afya yakabiliwa uhaba watumishi 53%

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema kwa sasa kuna uhaba wa watumishi wa kada za afya kwa asilimia 53.

Kutokana na hali hiyo, Kituo cha Udhibiti wa Magonjwa nchini Tanzania (CDC) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania kitasaidia kupunguza uhaba wa rasilimali watu wa kada hiyo kwa kutoa ajira za mikataba kwa Watanzania.

Waziri Ummy aliyasema hayo hivi karibuni alipofanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkazi wa CDC-Tanzania, Dk. Mahesh Swaminathan, katika Ofisi za Wizara jijini hapa.

Aliishukuru CDC kwa kuendelea kuwa mshirika wa karibu wa serikali na wizara hiyo kwa kutoa ushirikiano na msaada katika mapambano dhidi ya magonjwa mbalimbali ikiwamo virusi vya Ukimwi, kifua kikuu, malaria pamoja na UVIKO-19.

"CDC amekuwa mshirika wetu wa karibu katika mapambano dhidi ya magonjwa mbalimbali na katika kutekeleza afua za kuboresha ubora wa huduma za afya nchini Tanzania," alisema.

Hata hivyo, alitaka ushirikiano zaidi katika kuboresha na kuongeza huduma za maabara za afya ya jamii pamoja na kuboresha mifumo ya ufuatiliaji wa magonjwa ili serikali kuchukua hatua stahiki mapema zaidi na kuokoa maisha ya wananchi. Pia, Waziri Ummy aliishukuru Serikali ya Marekani kupitia miradi na programu zinatokelezwa hapa nchini kwa kutoa msaada wa Dola za Marekani milioni 22 kwa ajili ya kusaidia serikali katika mapambano dhidi ya UVIKO-19 na kuhamasisha wananchi kuchanja zaidi chanjo ya ugonjwa huo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkazi wa CDC nchini, Dk. Swaminathan, aliishukuru Tanzania kupitia wizara hiyo kwa kuendelea kuwapa mazingira rafiki na ushirikiano zaidi katika kupambana na kudhibiti magonjwa.

"CDC imekuwa ikifanya kazi kwa ukaribu na Wizara ya Afya nchini katika mapambano dhidi ya VVU kwa kutoa msaada wa dawa za kupunguza makali ya virusi hivyo, kushiriki katika utafiti mbalimbali wenye kulenga kupata tiba dhidi ya magonjwa mbalimbali pamoja na mapambano dhidi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu, Malaria pamoja na ugonjwa wa UVIKO-19 nchini," alisema.

Alisema milango ya CDC ipo wazi muda wote kwa kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na rasilimali katika kusaidia serikali kutoa huduma bora za tiba kwa wananchi.



Mjasiriamali wa vikapu Hamida Jumaa (60) mkazi wa Chang'ombe Jiji la Dodoma akitafuta wateja barabara ya Nyerere kikapu kimoja anauza shilingi elfu tano. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mbunge aiomba serikali walimu 1,380

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu ameiomba serikali mambo sita katika jimbo hilo ikiwamo upatikanaji wa walimu 1,380 ili kukidhi upungufu uliopo.

Akichangia mwishoni mwa wiki bungeni katika makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI) kwa mwaka 2022/23, Mtaturu alisema mahitaji yaliyopo ni walimu 2,685 na waliopo ni 1,305 hali inayosababisha kutokuwapo kwa uwiano wa walimu na wanafunzi.

Alisema baadhi ya shule za msingi kuna walimu watano huku wanafunzi wakiwa zaidi ya 700.

"Sisi katika Halmashauri ya Ikungi tuna upungufu wa walimu wengi sana tuna upungufu wa 1,380, leo tunataka ufaulu upande, lakini hatuwezi kupandisha ufaulu huo bila ya kuwa na walimu wakutosha na katika hali hii tusitegemee mapinduzi ya elimu katika nchi yetu," alisema.

Alisema katika mwaka mmoja halmashauri hiyo imepokea zaidi ya Shilingi bilioni saba.

"Fedha hizi za maendeleo ni nyingi na tunaona zipo katika meneo mbalimbali ya vijiji vyetu, tumeona jambo kubwa la kujenga madarasa 67 na tulipata Sh. bilioni 2.6 ni fedha nyingi kwa wakati mmoja, tunashukuru sana na tunaipongeza serikali kwa mapinduzi makubwa katika elimu kwenye halmashauri yetu," alibainisha.

Aliishukuru serikali kutoa Sh. milioni 500 ambazo zimetumika katika ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Ntuntu na kitakapokamilika kitaondoa adha ya wananchi kutembea umbali mrefu.

"Katika kata 13 zilizopo katika jimbo letu, tumepata kituo hicho kimoja, hivyo niombe kupitia bajeti hii tukipata vituo hivyo vingine vitatu tutakuwa tumegusa maisha ya wananchi wa Misughaa, Mang'onyi na Issuna," alisema.

Kuhusu barabara, Mtaturu aliomba kuwe na mpango maalum wa kujenga madaraja na vivuko ili kusaidia barabara zinazojengwa vijijini zikamilike kwa wakati.

"Kwenye barabara tumepata Sh. bilioni 1.5 na imeleta mabadiliko makubwa na tunaipongeza serikali, lakini kwa barabara za vijijini ambazo tunahitaji vivuko na madaraja, na bajeti hatutengi tutakuwa tunategemea kitu ambacho hatujakipanga."

"Ingekuwa vizuri fedha za maendeleo zinatoka moja kwa moja TARURA tunatenga kwa ajili ya vivuko na madaraja ili mameneja wa wilaya wabaki kwenye eneo la kutengeneza barabara na matuta, lakini ukisema leo afanye kazi ile ile usitegemee mabadiliko ya barabara katika halmashauri zetu," alisisitiza.



# Walalamikia uongozi wa TAZARA kutotoa ushirikiano

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

VIONGOZI wa Kata ya Mswiswi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamewalalamikia viongozi wa Shirika la Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), wanaosimamia kiwanda cha kokoto cha Kongolo Mswiswi wakidai hawana ushirikiano na jamii inayowazunguka.

Viongozi hao walitoa tuhuma hizo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, aliyetembelea kiwanda hicho kwa lengo la kukagua mitambo iliyonunuliwa na TAZARA ambayo Kamati ya Bunge ililalamika baadhi ya mitambo hiyo kuwa mibovu.

Diwani wa Kata ya Mswiswi, Elia Bange, alitoa malalamiko hayo mbele ya Naibu waziri akidai uongozi wa Shirika hilo haushirikiani na wananchi na kiwanda hicho hakichangii shughuli za maendeleo.

Bange alisema uongozi wa shirika hilo una urasimu ambao unasababisha vijiji vinavyouzunguka mgodi huo kutonufaika na wamekuwa wakiomba baadhi ya vitu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, lakini hawapewi ushirikiano.

"Hivi karibuni tulikuwa na ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule yetu ya sekondari, tuliomba kokoto hapa wakatunyima tukalazimika kwenda kuomba kwenye mgodi mwingine ambao upo nje ya eneo letu na huko walitupatia na wakatusafirishia bure," alisema Bange.

Alisema pia, amekuwa akipokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wafanyakazi wa kiwanda cha kokoto wakilalamikia mazingira magumu ya kazi.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Kongolo Mkola, George Myaba, alisema wanapohitaji kitu chochote kutoka kwenye kiwanda hicho hutakiwa kuandika barua na kuipeleka Makao Makuu ya TAZARA.

Alisema barua hizo hatahivyo, hazijibiwi na hata zikijibiwa sio kwa wakati hali ambayo inawakwamisha kwenye shughuli ambazo wanakusudia kutekeleza.

Alisema wakati mwingine wanapewa tofauti na mahitaji halisi ya miradi wanayotaka kuitekeleza hasa kwa kupewa kiwango ambacho hakiendani na makubaliano wanayoingia.

"Hivi karibuni tuliomba tani 150 za mawe kwa ajili ya ujenzi wa shule wakatupatia, lakini tulibeba tani 60 wakatusimamisha na mimi kama kiongozi niliamua kuwahamasisha wananchi wangu kwenda mlimani kupasua mawe," alisema Myaba.

Meneja wa mgodi wa kuzalisha kokoto wa kiwanda hicho, Idd abdallah alikanusha tuhuma na kwamba wanashirikiana na wananchi kwenye shughuli mbalimbali wanazohitaji kushirikiana.

Alisema hivi karibuni alikuwa yuko safarini mkoani Dar es Salaam akapigiwa simu na viongozi wa kijiji wakiomba wasaidiwe baadhi ya vitu kwa kumwelekeza msaidizi wake awasaidie.

Hata hivyo, Naibu Waziri wa Ujezi na Uchukuzi, Mwakibete aliuagiza uongozi wa TAZARA kuimarisha ushirikiano na wananchi hao kabla ya Mei mosi, mwaka huu.

Aliagiza viongozi hao kuandaa mpango kazi wa namna sahihi ya kuendesha kiwanda hicho kwa faida na kwamba mpango kazi huo uambatane na maelezo ya kueleza namna ya kuimarisha ushirikiano na wananchi.



Mdau wa maendeleo wa mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela (kushoto), akimkabidhi Shilingi milioni moja Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Ayas Njalabaha. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mdau aichangia BAKWATA ujenzi wa ofisi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MDAU wa maendeleo wa Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, amechangia Sh. 1,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Baraza la Waislamu (BAKWATA), Mkoa wa Mbeya ambazo zinajengwa Sokomatola, jijini Mbeya.

Mwaselela aliukabidhi uongozi wa BAKWATA mchango huo mwishoni mwa wiki na kuahidi kusomesha watoto 10 wa familia hizo kidato cha tano na sita kama sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali.

Alisema ametoa mchango huo kama sehemu ya kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa na kabla ya kutoa mchango huo aliamua kutembelea taasisi mbalimbali za umma kwa ajili ya kutoa msaada wake.

Mwaselela ambaye pia ni Mkurugenzi wa Shule za Patrick Mission ya mkoani Dar es Salaam na Paradise Mission ya mkoani Mbeya, aliwashauri viongozi wa BAKWATA kuanzisha shule na kwamba yuko tayari kushirikiana nao kukusanya fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo.

"Mimi ni mkristo, lakini nimeamua kushirikiana nanyi kujenga nyumba hii kwa sababu wote tunamtafuta Mungu, lakini pia nilikuwa na shughuli zangu za kijamii tangu asubuhi hivyo nikaamua nije hapa nishirikiane nanyi maana sisi ni wamoja," alisema Mwaselela.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya waislamu wa Mkoa huo, Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Ayas Njalabaha, alimshukuru Mwaselela kwa msaada huo na kuwa kwa sasa jengo lao limefikia hatua za umaliziaji.

Alisema baraza hilo lina taasisi za elimu ikiwamo shule, lakini ni mpya na wanahitaji muda kuifanya ifahamike zaidi na kumuomba Mwaselela aendelee kushirikiana nao.

# Waliopata maafa kuezuliwa nyumba waomba msaada

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI Kijiji cha Holongo katika Kata ya Igale, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambao nyumba zao ziliezuliwa na mazao kuharibiwa kutokana na mvua iliyokuwa imeambatana na upepo na mawe, wameiomba serikali kuwasaidia ujenzi wa nyumba zao na chakula ili kupunguza hasara waliyoipata.

Mvua hiyo ilinyesha wiki mbili zilizopita na kwa mujibu wa wananchi hao ilinyesha kwa muda usiozidi saa moja na nusu, lakini ikaleta madhara kwa kuezua baadhi ya nyumba, kubomoa nyumba na mazao kuharibika.

Mmoja wa wananchi hao, Rebeca Wilson, alisema wakati mvua hiyo inaezua nyumba yake, alikuwa ndani na watoto wake wawili pamoja na wajukuu watatu na hakuna aliyepata madhara licha ya nyumba kuezuliwa na moja ya kuta kuanguka.

Rebeca alisema vitu vyake vyote viliharibika na hana chochote huku mazao aliyokuwa amepanda shambani yakiharibika na kuomba asaidiwe kupunguza hasara kwa kuwa bati zilizoezuliwa ziliharibika.

"Naomba wasamaria wema wanisaidie kuezeka nyumba yangu maana mabati yote yameharibika na hata chakula sina nahangaika sana, hata jiko ambalo nimehamia linavuja sana," alisema Rebeca.

Naye Enea Mwabhela alisema wakati nyumba yake inaezuliwa alikuwa amekaa ndani na watoto wake huku mume wake ambaye ana ulemavu akiwa amelala chumbani.

Alisema mabati ya nyumba hiyo yaliezuliwa na kupelekwa umbali wa zaidi ya mita tano kutoka ilipo nyumba hiyo hali ambayo ilisababisha zikaharibika na hazifai kutumika tena.

Alisema alihamia kwenye pagala pamoja na familia yake na kwamba nyumba hiyo ni ndogo haifai kuishi na familia kubwa.

"Chakula chote kiliharibika na nimekuwa na mzigo mkubwa maana majukumu yote ya familia yananikabili mwenyewe, mume wangu hana kazi yoyote kwa sababu ni mlemavu wa mkono mmoja ambao ulikatwa," alisema Enea.

Alisema jiko walilohamia limebomoka ukuta mmoja hali inayosababisha hatari kwa maisha yake na familia nzima.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Meshack Mayasu, alisema kijiji hicho kina vitongoji vinane, lakini vilivyoathirika na mvua hiyo ni vitongoji sita na viwili pekee ndivyo vilivyopona.

Alisema mazao yaliyoathirika ni mahindi, kahawa na maharagwe ambayo alisema yalikuwa bado hayajakomaa na kuna hatari wananchi hao wakakumbwa na njaa pamoja na kuporomoka kiuchumi.

Pia, ili kukabiliana na ukali wa maisha wanawaomba wadau mbalimbali ikiwamo serikali kuwasaidia wananchi hasa ambao nyumba zao zimeezuliwa wasaidiwe.



## Wanolewa kukabili athari za tabianchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANAFUNZI wa Shule ya Lauret Zanzibar, wamepewa mafunzo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kuwa mabalozi wazuri kwa jamii.

Wanafunzi hao wamepewa elimu hiyo na umoja wa kampeni ya elimu ya mabadiliko ya tabianchi Zanzibar (Frigays for future Zanzibar) ili kuongeza uelewa kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza na wanafunzi wa kidato cha nne wa Shule hiyo iliyoko Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar, Khatib Hamad Kombo, mjumbe wa kampeni hiyo, alisema tatizo la mabadiliko ya tabianchi ni la kidunia na ili kupata maendeleo endelevu lazima kukabiliana na mabadiliko hayo kwa kutunza mazingira.

"Ili kupata maendeleo endelevu na uchumi wa nchi kukua kwa kasi lazima tupambane na mabadiliiko ya tabianchi na kuepukana na athari ambazo zipo ikiwemo kutokata miti ovyo, kutotumia rasilimali ambazo hazifai,"alisema.

Alisema harakati zao za kutoa elimu hiyo ni kuunga nguvu jitihada ya serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kupata maendeleo endelevu.

Aidha aliitaka jamii kulinda mazingira kwa kupanda miti na kutumia gesi kwa kupikia ili kutochafua mazingira kwa kuwa miti mingi hukatwa kwa ajili ya harakati za kijamii ikiwemo kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia.

Kwa upande wao wanafunzi wa Shule hiyo, walisema kuwa elimu waliyopatiwa wataifanyia kazi ili kulinda mazingira na kuepukana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mmoja wa wanafunzi hao, Hannan Said, alisema kuwa watahakikisha wanazitumia taka za plasitiki kwa matumizi mbadala badala ya kuzituma au kuzichoma moto ili kulinda mazingira.

Naye Mwalimu wa Shule hiyo Omar Hamad, aliwataka wanafunzi hao kuyafanyia kazi mafunzo hayo waliyopewa ili kuwa mabalozi wazuri kwa jamii na kuzitaka taasisi zingine kufika shuleni hapo kwa ajili ya kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira.

"Wanafunzi hawa ndio viongozi wa baadae hivyo ni vyema elimu ya utunzaji wa mazingira kutolewa shuleni ili kuwa na uelewa mzuri kwa faida yao na nchi kwa ujumla, "alisema Mwalimu huyo.

# Mwanaharakati aingilia kati mgogoro wawekezaji hoteli

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAHARAKATI wa Haki za Binadamu na Utawala Bora Zanzibar, Ali Issa Makame, amesema kuna uvunjaji wa sheria za ukodishwaji wa hoteli kati ya wawekezaji wageni wanaokodishwa kuendesha hoteli na wamiliki wazalendo visiwani Zanzibar.

Makame aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kufuatia mgogoro uliojitokeza kati ya mmiliki wa hoteli ya Sipano Beach Lorge, Peter Sipano Ole Meelt na muwekezaji aliyekodishwa kuendesha hoteli hiyo Erkan Acikel raia kutoka nchini Uturuki.

Alisema migogoro kati ya wawekezaji wazalendo na wageni imeanza kujitokeza kwa wingi katika sekta ya utalii na kuathiri maendeleo ya wawekezaji wazalendo ambao wamewekeza katika ujenzi wa hoteli na kuwakaribisha wawekezaji kutoka nje kuendesha hoteli lakini imekuwa kikwazo cha maendeleo ya miradi yao.

"Tunaomba serikali kuchunguza kwa kina migogoro inayoendelea kujitokeza kati ya wawekezaji wazalendo na wageni waliokodishwa kuendesha hoteli na baadae kushindwa kuheshimu mikataba na kushindwa kulipa gharama za makubaliano,"alisema Makame.

Aliongeza kuwa imefikia hatua wawekezaji wanashindwa kuheshimu uamuzi wa mahakama na watendaji katika ngazi ya sekta ya utalii wakiwemo kamisheni ya utalii na mamlaka ya uwekezaji Zanzibar (ZIPA)

Vilevile Makame alieleza kuwa Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi, ameonesha nia yake ya kutetea wanyonge na kusimamia haki na viongozi waliopewa dhamana wanapaswa kuunga mkono juhudi zake ili kuhakikisha haki inatendeka kwa wawekezaji wazalendo, wafanyakazi katika sekta ya utalii na wasambazaji wa vyakula katika sekta hiyo.

Alisema kuwa pamoja na Mahakama Kuu Zanzibar kutoa amri ya kuwataka wawekezaji hao kuondoka katika hoteli hiyo baada ya mkataba wao kumalizika bado wameendelea kugoma bila ya kuchukuliwa hatua yoyote ya kisheria jambo ambalo linakwenda kinyume na misingi ya utawala bora.

"Zanzibar inaongozwa kwa misingi ya utawala wa sheria haiwezekani amri za mahakama zikavunjwa bila ya wahusika kuchukuliwa hatua lakini jambo hili halileti sura nzuri katika mitazamo ya haki za binadamu na utawala bora,"alisisitiza Mwanaharakati huyo.

Sheha wa Kiwengwa, Maulid Masoud Ame, alisema amepokea malalamiko kuhusu mwekezaji huyo kuwa amemaliza mkataba wa ukodishwaji lakini amegoma kurejesha hoteli hiyo.

"Malalamiko ya kesi hii ninayo, muendeshaji wa hoteli raia wa Uturuki muda wake wa ukodishwaji umemalizika lakini amegoma kuondoka kwenye hoteli na amevunja masharti ya mkataba na mmiliki mzalendo wa hoteli hiyo,"alisema.

Alieleza kuwa hatua alizozichukua ni kuripoti katika mamlaka dhamana za kusimamia sekta ya utalii baada ya kuona taratibu za kisheria zinashindwa kuzingatiwa na wawekezaji hao raia wa Uturuki bila ya kuchukuliwa hatua za kisheria, licha ya amri za mahakama kuu kutolewa za kuwataka kuondoka katika eneo hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari, mmiliki wa Hoteli hiyo, Peter Sipano Ole Meelt, alisema mwekezaji huyo alimkodisha hoteli yake kwa muda wa miezi sita kwa gharama za malipo ya Dola 60,000 ambapo kwa kila mwezi dola 5000.

"Mkataba ulianza Agosti mwaka jana lakini tangu kumalizika Febuari mwaka huu hawataki kurejesha hoteli na wameshindwa kuzingatia masharti ya makubaliano ya kufanyia matengenezo hoteli na mpaka sasa hoteli ipo katika mazingira chakavu kinyume na masharti ya mkataba,"alisema muwekezaji huyo mzalendo.

Peter alisema muwekezaji huyo amekuwa akilindwa na mteule mmoja wa rais na kuomba Rais wa Zanzibar kuchunguza mgogoro huo ili haki itendeke baada ya raia hao wa Uturuki kugoma kurejesha hoteli na kuanza kumbambikizia kesi za jinai mmiliki wa hoteli aliyewakodisha.



Mwanaharakati wa Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ali Makame Issa, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tatizo la baadhi ya wawekezaji katika sekta ya utalii kutoheshimu mikataba ya uendeshaji wa hoteli na kuwaathiri wamiliki wa hoteli wazalendo Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu wa Rais ataka umeme Pujini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ametoa wiki mbili kwa Shirika la Umeme Zanzibar ofisi ya Pemba kuhakikisha wanasogeza huduma ya umeme katika kijiji cha Pujini ili kurahisisha kukamilika kwa miradi ya maendeleo iliyopo eneo hilo.

Hemed alitoa agizo hilo jana wakati akikagua miradi inayojengwa kwa fedha za kupunguza athari za UVIKO-19 katika Mkoa wa Kusini Pemba.

Alisema serikali imetoa maelekezo ya kumaliza changamoto zote za kimiundombinu ikiwemo umeme na maji katika maeneo yanayojengwa miradi mbalimbali ili makandarasi wasikutane na changamoto ya aina yoyote.

Alisema ni vyema makandarasi na wizara zilizopata miradi kutoka katika fedha za UVIKO -19 kuhakikisha wanakaa pamoja na taasisi mbalimbali ili kutoathiri miundombinu iliyopo katika maeneo ya miradi hiyo.

Vilevile Hemed aliutaka uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Kusini Pemba kuhakikisha wanalipima eneo hilo kujua ukubwa wake na kuwahakikishia wanachi wa mkoa huo kuwa eneo hilo linakamilika ili kuwawekea mazingira rafiki wajasiriamali wadogo.

Aidha makamu wa rais huyo ameonesha kutoridhishwa kwake na baadhi ya makandarasi walio nje ya muda wa makubaliano katika mikataba na kueleza kuwa serikali imedhamiria kurejesha heshima katika ujenzi wa miradi mbalimbali na kuwataka makandarasi hao kuheshimu mikataba yao.

Aidha aliwasisitiza makandarasi hao kuhakikisha wanaendeleza ushirikiano na wananchi walio katika maeneo husika na kueleza kufurahishwa kwake kuona wakaazi wa maeneo hayo wanapata ajira katika ujenzi wa miradi hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Matar Zahor Masoud, alifurahishwa na hatua ya serikali kwa kutenga fedha kwa miradi mbalimbali katika mkoa huo.

Alieleza kuwa ni wajibu wao kusimamia miradi hiyo kwa kuwa karibu na makandarasi kwa kutatua changamoto zinazowakabili katika miradi hiyo ili kukamilika kwa wakati na kwa kiwango kinachohitajika.

Ziara hiyo ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mkoa wa Kusini Pemba inakamilisha ziara alizozifanya katika Mikoa yote ya Zanzibar na kujionea namna miradi hiyo inavyoendelea kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

# Uzembe wa madereva watajwa kichocheo kikuu cha ajali Z'bar

**Na Christina Mwakangale**

ASILIMIA 48 ya wahojiwa kuhusu ajali za barabarani, kisiwani Zanzibar, wameeleza kwamba uzembe wa madereva ni kati ya chanzo kikuu cha ajali za barabarani, huku asilimia 27 wakisema ni kutozingatiwa sheria za barabarani.

Takwimu hizo zimebainishwa hivi karibuni mkoani Dar es Salaam, kwenye uzinduzi wa Ripoti ya Haki za Binadamu 2021, iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Huduma za Kisheria Zanzibar (ZLSC), Harusi Mpatani, alisema hali hiyo inasababisha kuondolewa haki ya kuishi kutokana na ongezeko la ajali huku sababu baadhi zikitokana na uzembe wa kibinadamu.

Alisema ZLSC kwa kushirikiana na taasisi ya kupambana na changamoto za vijana Zanzibar (ZAFAYCO), mwaka 2021, ilifanya utafiti kuhusu haki za binadamu, haki ya kuishi, ilibaini hayo.

"Asilimia 19 walitaja mwendokasi ni chanzo cha ajali na asilimia tatu tu ya waliohojiwa walitaja ubovu wa miundombinu ya barabara, huku wengine asilimia tatu walitaja sababu nyingine na moja walisema hawajui," alisema Harusi.

Pia, Harusi alitaja ongezeko la matukio ya kujichikulia sheria mkononi huku kesi za mauaji zikiwa hazina mwendelezo na pia kwenye haki ya elimu akieleza usawa bado, na kwamba wanafunzi kwenye baadhi ya skuli hukaa chini na wengine kulazimika kutumia vyoo vichache licha ya wingi wao.

"Haki ya afya, pamoja na jitihada za mwaka jana, kuna changamoto bado, kuna upungufu wa madaktari, wauguzi na ma-specialist, ni wachache na kusababisha wagonjwa kuja Dar es Salaam, kupata tiba.

"Dawa pia ni changamoto , kuna hospitali au wananchi walikosa dawa muhimu hii inaweza kusababisha haki ya afya kuvunjwa. Uviko-19 pia imesababisha haki ya afya kupungua kwa kuwa suala la ubaguzi lilichukua nafasi kubwa.

"Iwapo mgonjwa aliyeugua akifika hospitalini iliangaliwa huyu ni nani hakukuwa na usawa hii iliweza kupunguza haki ya afya."

Harusi alibainisha kuwa, ukatili wa kijinsia (GBV), umeripotiwa mara kwa mara visiwani humo, akisema ubakaji kipindi cha mwaka 2021, uliongezeka kuripotiwa hasa kwa watoto na wanawake.

"Asilimia 47 wanazungumza kwamba matukio yapo katika jamii. Asilimia 29 ya ndoa za utotoni. Mkoa wa Mjini Magharibi, huripotiwa zaidi matukio ya GBV. Pia kuna upungufu wa kuwasaidia watoto kisheria waliofanya makosa, wakienda mahakamani hii inawanyima haki kisheria," alieleza Harusi, akiongeza:

Bado kuna msongamano kwenye magereza na kukosekana kwa dhamana ni tatizo Zanzibar, hasa kwa makosa yahusuyo GBV."

Alisema utafiti huo wa haki za binadamu ulijikita katika maeneo tofauti, ikiwamo vurugu za makundi, haki ya watoto, haki ya jinai, upatikanaji wa haki, ajali za barabarani.



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela (kushoto) akisalimiana na Askofu Mteule wa Kanisa la Moravian , Jimbo la Mashariki, Mchungaji Lawi Mwankuga mara baada ya kuhitimisha ibada ya Pasaka iliyofanyika kitaifa katika kanisa hilo la Moravian Usharika wa Morogoro juzi. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

## Mbunge mstaafu wa CHADEMA afuturisha wafungwa na mahabusi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MOSHI

MBUNGE mstaafu wa Jimbo la Moshi mjini, kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA),Jafari Rafael Michael, ametoa misaada mbalimbali ya vyakula kwa wafungwa na mahabusi wa gereza kuu la Karanga lililopo mjini Moshi.

Vyakula vilivyotolewa ni mchele kilo 250, mafuta ya kula lita 40, unga wa ngano kilo 50, tambi pamoja na vitu vingine vya kufuturia.

Jafari aliwatembelea wafungwa wa gereza hilo ikiwa ni sehemu ya kurudisha katika jamii kile anachokipata katika utekelezaji wa majukumu yake.

Akikabidhi misaada hiyo kwa niaba ya mbunge huyo wa zamani Katibu wake Deogratius Kiwelu, alisema imekuwa ni kawaida yake kutoa futari kwa wafungwa na mahabusi, kama sehemu ya sadaka yake katika kipindi hiki cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

"Kwa niaba ya Jafari, tumefika hapa kuwasalimu wafungwa na mahabusu hawa, pamoja na kuwafariji, lakini pia tumewaletea mahitaji mbalimbali ikiwemo vyakula mbalimbali kwa ajili ya futari, kama ambavyo tunafahamu huu ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani,"alisema Kiwelu.

Aidha, Kiwelu alitoa wito kwa wadau wengine kujitokeza kusaidia wahitaji mbalimbali katika jamii, ili kuwawezesha kukabiliana na changamoto za maisha wanazopitia.

Alisema wahitaji katika jamii ni wengi, wakiwemo watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, wasiojiweza, yatima na watoto wanaoishi na kulelewa katika vituo vya watoto wa mitaani, hivyo jamii ione umuhimu wa kuwasaidia ili kufikia ndoto zao za kimaisha.

Akizungumza kwa niaba ya wafungwa wenzake, ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alimshukuru Jafari kwa kuwatembelea na kuwaletea mahitaji hayo huku akiomba kutochoka kuwatembelea na kuwasaidia kutatua changamoto zao.

# Wafugaji walia na matapeli wa mifugo Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

WAFUGAJI wa kuku wa kisasa Kiwani Wilaya ya Mkoani wamelalamikia kuwapo kwa matajiri wanaojifanya kutaka kuwasaidia lakini mwishowe huwatapeli pesa zao.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa wafugaji hao, Abdalla Rukuni, alisema kuwa yeye na wafugaji wengine waliingia ubia na matajiri wa eneo hilo kwa lengo la kuwaongezea mitaji lakini baada ya kuuza kuku hao matajiri hao hawakuwalipa stahiki zao.

"Mkataba wetu ni kwamba sisi tuna kuku wetu wenyewe na mashine zetu lakini wao walikuja tukakubaliana na tukajenga mabanda, sasa sijui ilikuwa ni kwa hadaa au vipi", alisema mfugaji huyo.

Alieleza kuwa, baada ya kukubaliana walikwenda kujenga mabanda makubwa matatu yenye uwezo wa kuingiza kuku 740 kwa kila banda.

Alisema, muhisani huyo alianza kuwaletea chakula cha kuku kutoka Tanga na wakaanza kuzalisha mpaka mabanda yao yakajaa na hivyo kuwalazimu kuongeza mashine nyingine za kutotolesha vifaranga kwa kuwa hizo tatu walizokuwa nazo zikawa hazitoshi.

"Tuliwasambaza kwa wafugaji wenzetu maeneo tofauti, tuliwajengea mazingira mazuri na wakaanza kufuga kwa mkataba pia, tulifikia pahali mpaka mimi nilikwenda Unguja kuchukua kibali cha kusafirisha lakini baada ya kuuza kuku, sisi hatukurudishiwa chochote", alisema.

Kwa upande wake Rehema Kassim Mohamed alieleza kuwa, hawakupewa mrejesho wowote baada ya mauzo, jambo ambalo lilisababisha wafugaji kusambaratika na kila mmoja kuendeleza mwenyewe kama ilivyokuwa zamani.

Alisema kuwa walipogoma tajiri huyo alikwenda kutaka suluhisho lakini wafugaji hao waligoma kutokana na kutokuwa na imani nao tena kwa kuwa walipoteza mwaka mmoja bila kupata mafanikio yoyote.

"Kuku walikuwa ni wengi sana, kwa sababu sisi tulikuwa tunazalisha na kupeleka mashambani kwa wafugaji wengine, kwa kweli walituhudaa, hivyo tunawaambia na wengine wawe makini kwa hili", alieleza.

Mfugaji mwingine .Muna Abdalla alieleza kuwa, walianza kufanya shughuli zao za ufugaji kwa kutarajia kujiongezea kipato ingawa walirudi nyuma kwa kuwa ile idadi waliyokuwa nayo mwanzo imepungua sana.

"Sisi tulikuwa na kuku zaidi ya 6000 lakini kwa sasa banda zima nina kuku 500 tu, kwa kweli nimerudi nyuma kimaendeleo, kwa hiyo ninajifufua upya", alisema Abdalla Rukuni.

Mfugaji Najma Mohamed alisema kuwa kilichowaponza ni kutofunga mkataba kimaandishi na ndiyo maana hawakupata nguvu ya kufanya lolote, kwani ilikuwa wanauza kuku na vifaranga na fedha walikuwa wanamkabidhi tajiri wao kwa vile walimuamini.

"Ni tajiri kutoka hapa hapa kisiwani Pemba, jinsi alivyokuwa akituambia maneno mazuri na vile alikuwa ametuzidi umri, tulimuweka kama kiongozi na mlezi wetu", alisema.

UCHAGUZI MKUU KENYA 2022:

## 'Tumejiandaa kwa uchaguzi'

**Nairobi,** KENYA

WAZIRI wa Usalama, Dk. Fred Matiang'i, amewahakikishia Wakenya kwamba, uchaguzi wa Agosti, mwaka huu, utakuwa wa amani kwa kuwa wamejiandaa vyema ili kudumisha amani wakati na baada ya uchaguzi.

Akihojiwa na moja ya chombo cha habari, waziri huyo alipuuza madai ya watu kuwa huenda kukatokea wizi wa kura katika uchaguzi wa Agosti.

Amesema walianza kujiandaa kwa shughuli ya uchaguzi miaka miwili iliyopita.

"Maofisa walipelekwa katika maeneo mbalimbali ili kukagua na kuchunguza kwa kina dalili zozote za vurugu. Kufikia sasa, nawahakikishia Wakenya kuwa tumetembea kila mahali na hakuna ushahidi wa fujo," anasema Dk. Matiang'i.

Kuhusu maandalizi ya uchaguzi, Dk. Matiang'i, anasema kuwa sekta hiyo ina rasilimali za kutosha kuhakikisha kuwa shughuli ya uchaguzi inafanyika bila kuingiliwa kati.

Amesema kuwa huduma ya polisi ni huru na haitawaliwi na mwanasiasa yeyote.

"Maofisa wanafuata sheria zetu na nina imani kuwa watafanya juu chini ili kuwatumikia Wakenya kwa njia mwafaka. Sisi hatufuati hisia zetu bali tunatawaliwa na sheria," amesema Dk. Matiang'i.

Amesema maofisa wake hawana uoga wowote kuhusu nani atakayepata ushindi kwani kazi yao ni kuwatumikia Wakenya na kuhakikisha kuwa kuna amani.

Amesema nafasi yake kama Waziri haifai kumzuia kuhusika katika masuala ya siasa kwa kuwa ana haki kama wananchi wengine kumchagua kiongozi anayempenda.

"Mimi si mashine. Mimi ni binadamu na nina haki ya kumchagua kiongozi ninayempenda."

Amesema hana shida na atakayechaguliwa kuwa rais wa Kenya kwani kazi yake kama waziri ni kuhakikisha kuwa Wakenya wanaishi kwa amani kila wakati.

Dk. Matiang'i amesema kuwa ataendelea kuhudumu ikiwa atakayechaguliwa kuwa rais atampa nafasi hiyo.

"Mimi ni mwananchi na hivyo nitafanya kazi na atakayechaguliwa kuwa rais. Nitawatumikia Wakenya kama Waziri wa Usalama na Masuala ya Ndani ikiwa rais aliyechaguliwa atanipa nafasi hiyo," alihakikisha.

Kwa mujibu wa wadhifa wake, waziri huyo ni miongoni mwa Kamati ya Watu 22 ambayo itashughulika na mchakato wa kukabidhi mamlaka kwa rais atakayechaguliwa.

**• Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**



Wafanyakazi wa dharura, wakisafisha eneo lililoshambuliwa Magharibi mwa mji wa Lviv, nchini Ukraine, jana. Inakadiriwa watu sita wameuawa. **PICHA: AP**

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# Russia yalenga maghala ya kuhifadhia silaha

**Kyiv,** UKRAINE

NI siku ya 55 tangu Russia ilipotangaza mashambulizi dhidi ya Ukraine, huku miji kadhaa ikishuhudia mashambulio ya anga, usiku wa jana.

Mji wa Kharkiv, Zaporizhzhia, Donetsk na Dnipropetrovsk na bandari ya Mykolayiv ni kati iliyoshambuliwa jana.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskyy amesema pamoja na tangazo la Russia kwamba wanajeshi waliopo mji wa bandari, Mariupol wajisalimishe, amesema na kuahidi hawatokata tamaa.

Meya wa mji wa Lviv amedai mashambulizi eneo hilo yamesababisha vifo vya watu saba, huku vikosi vya Ukraine vikisema havitosalimu amri, vitasalia mji wa Mariupol.

Russia imedai kwamba imelenga maeneo takribani 100 na kuyashambulia usiku wa kuamkia jana kwenye mikoa tofauti ikiwamo sehemu za maghala ya silaha.

Vyombo vya habari vya serikali ya Russia vimeripoti, jeshi lake lilishambulia jumla ya malengo 315 nchini Ukraine usiku kucha na miji kadhaa ikishambuliwa Jumatatu.

Wizara ya Ulinzi ya Russia, ilisema kuwa imeharibu maghala manne ya silaha na vifaa vya kijeshi nchini Ukraine kwa makombora ya Iskander, kombora la masafa mafupi, shirika la habari la TASS limeripoti.

"Makombora ya anga ya juu yaliharibu vituo 16 vya kijeshi vya Ukraine usiku wa kuamkia leo," msemaji wa wizara ya ulinzi ya Russia Igor Konashenkov imesema.

Hata hivyo Yuri Sak, mmoja wa washauri wa Waziri wa Ulinzi wa Ukraine, ambaye yuko magharibi mwa Ukraine, amekuwa akizungumza kuhusu mashambulio katika mji wa Lviv.

"Kilichotokea leo ni kitu cha kutisha kwa sababu hili ni shambulio kubwa la kombora dhidi ya miundombinu ya kiraia."



Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky



Rais wa Urusi, Vladimir Putin

### UKRAINE YAKATAA KUONDOKA

Maofisa wa Ukraine wamekataa matakwa ya vikosi vya Russia, kuwa watetezi wa mji wa Mariupol wanapaswa kuweka chini silaha zao.

Waziri Mkuu wa Russia, Denys Shmyhal amesema katika mahojiano na ABC kwamba vikosi vya Ukraine ambavyo bado viko mjini vitapigana hadi mwisho.

Wanajeshi wa Kikosi cha Azov bado wamejificha kwenye jengo kubwa la chuma la Azovstal, Russia imetoa njia salama kwa wale wanaojisalimisha. Kuteka mji mzima kunaonekana kama zawadi kuu ya kimkakati kwa Russia, na kuiacha ikidhibiti eneo kubwa la Kusini na Mashariki mwa Ukraine.

Moto unasemekana kutanda katika jiji lote.

HABARI MICHEZO

TUMEWALIZA...




Wachezaji wa Mtibwa Sugar wakishangilia baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wenyeji Dodoma Jiji FC, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# ZIMAMOTO YAREJEA MAPEMA KUJIWINDA NA LIGI KUU, FA CUP

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MAAFANDE wa Zimamoto wameanza mazoezi kuelekea michezo ya Ligi Kuu Zanzibar ambayo itaendelea Mei 14, mwaka huu baada ya kumaliza mfungo wa Mwezi wa Ramadhani.

Ligi Kuu Zanzibar pamoja na ligi zote kisiwani hapa, zimesimama kupisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ikiwa ni utamaduni kwa Zanzibar ligi kusimama Mwezi wa Ramadhani unapoingia.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohammed Hilali 'Kocha Teddy', alisema kikosi hicho kil ianza rasmi mazoezi jana baada ya ma pumziko mafupi tangu ibada ya funga ilipoanza.**

Alisema katika kipindi hiki cha Ramadhani, timu hiyo itakuwa inafanya mazoezi yake mara moja kwa siku majira ya asubuhi pekee.

Alisema kuanza mapema kufanya mazoezi kwa kikosi chake hicho kunatokana na kujiandaa na michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, baada ya kujitoa katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu.

" Tumeanza mazoezi leo Jumatatu (jana), tumejikita na maandalizi ya michuano ya FA ambayo tumeingia nusu fainali, lakini pia na michezo ya ligi ili mechi zilizobaki tumalize vizuri," alisema.

Alisema licha ya kujitoa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, lakini malengo yao ni kuhakikisha michezo mitano iliyobaki wanamaliza kwa kupata matokeo mazuri.

Timu ya Zimamoto ipo nafasi ya sita ikiwa na alama 43 katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar , wakati kwenye michuano ya Kombe la FA imetinga hatua ya nusu fainali na itacheza mechi ya kwanza Mei 10, mwaka huu

# Vivier aanika malengo Biashara Utd

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Vivier Bahati, amesema ataendelea kuwapa mbinu zaidi wachezaji wake ili kuhakikisha wanashinda mechi 11 za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara walizobakiza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Vivier alisema moja ya masharti na vigezo walivyowekeana na uongozi wa Biashara United ni kuhakikisha timu inaendelea kubaki na kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Alisema awali timu ilikuwa katika hali mbaya ikishika nafasi ya chini, lakini kwa sasa amekiboresha kikosi chake kwa kuwajenga wachezaji aliokuwa nao, hivyo kumudu kupanda hadi nafasi 10 katika msimamo wa ligi hiyo.

"Kilichonileta Biashara United ni kuhakikisha timu haishuki daraja, nina matarajio makubwa hilo halitatokea kwa sababu nahitaji kupambana kuhakikisha nakisuka kikosi kuwa imara kwa ajili ya mechi 11 za duru la pili kufanya vizuri," alisema Vivier.

Alisema anafurahi kuona kikosi chake kina mabadiliko makubwa tofauti na mara ya kwanza alivyokikuta na anatumai watakuwa bora na kufikia malengo yao ya kuendelea kufanya vizuri katika michezo hiyo.

Biashara United inashika nafasi ya 10 ikiwa na pointi 22 katika msimamo wa ligi hiyo na Aprili 28, mwaka huu itakuwa na kibarua ugenini dhidi ya Mbeya City katika Uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya.

# Polisi Tanzania kambini leo

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la Ufundi la Klabu ya Polisi Tanzania, limesema timu yao inatarajia kurejea kambini leo baada ya kumaliza mapumziko mafupi.

Akizungumza na gazeti hili jana moja kwa moja kutoka Moshi mkoani Kilimanjaro, Kocha Msaidizi wa klabu hiyo, George Mketo, alisema Jumatano wataanza maandalizi ya mchezo dhidi ya maafande wenzao wa Tanzania Prisons utakaopigwa Mei Mosi, mwaka huu.

"Tuliwapa mapumziko mafupi wachezaji wetu mpaka Jumatano ili kuiweka sawa miili yao, ambapo watarejea kuanza mazoezi rasmi," alisema Mketo.

Kocha huyo alisema wanatambua mechi hiyo itakuwa ngumu, hivyo wataingia kwa tahadhari kubwa lengo likiwa ni kusaka ni kuhakikisha wanaondoka na pointi tatu katika mchezo huo.

Mchezo uliopita timu hiyo ilipata sare ya kufungana bao 1-1 dhidi ya Mbeya Kwanza FC.

Polisi Tanzania ipo nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 25 ilizojikusanyia katika michezo 20 iliyocheza hadi sasa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MANE NA MKATABA LIVER**
LIVERPOOL wanapanga kumpatia mkataba mpya mchezaji wa kimataifa wa Senegal, Sadio Mane. Mkataba wa sasa wa mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 30, unamalizika mwakani. (*Football Insider*)

**MODRID KUSTAAFIA MADRID**
KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amesema kiungo wa kati wa Croatia, Luka Modric atamalizia soka lake katika klabu hiyo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 amehusishwa na uhamisho wa kwenda Newcastle na Manchester City. (*Sun*)

**ARSENAL, INTER KWA NKUNKU**
ARSENAL huenda wakamkosa kiungo wa kati wa RB Leipzig, Christopher Nkunku baada ya Inter Milan kuongeza juhudi za kumpata Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 24. (*Gazzetta dello Sport*)

**GAVI AWINDWA LIVERPOOL**
LIVERPOOL wamempigia simu kiungo wa kati wa Barcelona na Hispania, Gavi mwenye umri wa miaka 17, kuhusu uwezekano wa kujiunga nao majira ya joto. (*Sport*)

**HAALAND HAENDI CITY**
MTENDAJI wa Borussia Dortmund, Sebastian Kehl amesema Manchester City hawajafikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wao raia wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21. (*Mail*)

**BERNARD ATAKIWA WEST HAM**
WEST Ham wako tayari kutoa dau la kumnunua mlinzi wa Manchester United, Di'Shon Bernard mwenye umri wa miaka 21, ambaye kwa sasa anaichezea Hull kwa mkopo. (*Mirror*)

**ERIKSEN KURUDI SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia mchezaji wao wa zamani na kiungo wa kati wa sasa wa Brentford, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 30. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark anapania kurejea Spurs. (*Football Insider*)

**ZHEGROVA AWINDWA ARSENAL**
KLABU ya Arsenal inapanga kumnunua winga wa Lille, Mkosovo Edon Zhegrova mwenye umri wa miaka 23. (*Sky Sports, via Teamtalk*)

**BAYERN HAIMUWEZI HAALAND**
MTENDAJI Mkuu wa Bayern Munich, Oliver Kahn amesema klabu hiyo haina uwezo wa kifedha kumsajili Erling Haaland. Kahn pia amethibitisha kuwa hawapo kwenye mazungumzo ya kuingia mkataba mpya na mshambuliaji wa timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33. (Sport, via *90 Min*)

**RICHARLISON KUSEPA EVERTON**
MSHAMBULIAJI wa Everton na Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 24, amewataka mawakala wake kumtafutia klabu mpya. (*Football Insider*)

**NEWCASTLE KUMRUDIA BREMER**
KLABU ya Newcastle inajiandaa kufufua tena mpango wao wa kumsaka beki wa Torino, Gleison Bremer. Kiungo huyo wa Brazil mwenye umrri wa miaka 25 pia ananyatiwa na Arsenal na Tottenham. (*Tuttomercato*)

## DONDOO ZA SOKA
### MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL AIHOFIA LIVER FAINALI KOMBE LA FA

Tulipoteza fainali ya Kombe la Carabao dhidi yao, tunapaswa kujiandaa vema dhidi ya moja ya timu kali zaidi...

**LONDON,** ENGLAND

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amewaambia waandishi wa habari hawavutiwi na Liverpool kuwinda mataji manne msimu huu, na pia alimsifia Timo Werner kwa kuwawezesha 'Blues' hao kupata ushindi wa mabao 2-0 kwenye nusu fainali ya FA dhidi ya Crystal Palace.

Chelsea walidhibiti muda wote, kwa kumiliki mpira kwa asilimia 67 na kupiga mashuti mara mbili, lakini hawakufunga bao hadi dakika ya 65 kupitia kwa Ruben Loftus-Cheek, kabla ya Mason Mount kuongeza la pili dakika ya 76.

Kwa ushindi huo, wamepata nafasi ya kucheza fainali ya Kombe la FA dhidi ya Liverpool kwenye Uwanja wa Wembley Mei 14, mwaka huu.

Huu ni msimu wa tatu mfululizo kwa Chelsea kuingia fainali, wakifungwa 2-1 na Arsenal mwaka 2020, na kufungwa 1-0 dhidi ya Leicester City mwaka 2021.

**Liverpool bado wako hai katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya, na wali washinda Chelsea kwa mikwaju ya penalti katika Kombe la Carabao, lakini Tuchel hakutaka kuzungumzia msimu wao ambao ungeweza kutengeneza historia.**

"Sijali kuhusu mataji mengine ya (Liverpool)," alisema.

"Bila shaka, tulipoteza fainali (ya Kombe la Carabao) (kwa Liverpool). Tulitoa kila kitu katika fainali hiyo, kama unavyojua, hadi penalti ya mwisho kabisa.

"Tulikuwa na bahati mbaya na tulipoteza. Tunataka kubadilisha mambo, lakini haitaturudishia taji la Carabao.

"Tulikuwa kwenye fainali ya Kombe la FA msimu uliopita na tuko hapa tena, ina maana kubwa sana kwetu.

"Tutakuwa tumejiandaa vema dhidi ya moja ya timu kali zaidi duniani, ambazo ziko katika kiwango bora kutokana na matokeo yao... itakuwa ngumu, (lakini) tutajaribu kufanya maisha kuwa magumu kwao."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,171

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 1.39
X | 4.85
2 | 6.54

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# HAKIMI AMTAKA MBAPPE ABAKI PSG

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Achraf Hakimi alimsifu mchezaji mwenzake Kylian Mbappe kama "mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani" na anatumai mshambuliaji huyo atabaki katika klabu hiyo.


Hata hivyo, mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco alisema atamuunga mkono Mbappe katika uamuzi wowote atakaofanya mwishoni mwa msimu huu, huku mkataba wa mshambuliaji huyo ukitarajiwa kumalizika Juni.

Katika mashindano yote, Mbappe amefunga mabao 31 na asisti 18 - kwenye mechi 39 msimu huu huku PSG ikikaribia kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Klabu hiyo ilikumbwa na hali mbaya ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid mwezi uliopita, na kuendeleza uvumi kwamba Mbappe anaweza kuondoka Paris na kujiunga na 'Los Blancos' mkataba wake utakapokamilika.

Hakimi anatamani sana kuona Mbappe akiongeza muda wake wa kukaa kwa miaka mitano katika mji mkuu wa Ufaransa.

"Mbappe ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani na ni rafiki yangu," alisema Hakimi akiiambia Telefoot.



# Ancelotti: Hakuna wa kutuzuia ubingwa LaLiga

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amekiri Real Madrid "wanakaribia" kunyakua taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya ushindi mnono dhidi ya Sevilla, Jumapili.

Sevilla walionekana kuwa na uhai katika mbio za LaLiga walipojikuta wakiwa mbele kwa mabao 2-0 yaliyofungwa na Ivan Rakitic na Erik Lamela.

Hata hivyo, uamuzi wa mwamuzi Guillermo Cuadra Fernandez kutotoa kadi ya pili ya njano na kumtoa Eduardo Camavinga kwa faulo yake mwishoni mwa kipindi cha kwanza kulileta madhara makubwa.

Camavinga alitolewa nje na nafasi yake kuchukuliwa na Rodrygo Mbrazil na akafanya jambo kwa haraka, akarudisha bao moja mapema kipindi cha pili.

Nacho Fernandez aliisawazishia Madrid dakika nane kabla ya mchezo kumalizika na kisha Karim Benzema akafunga bao ambalo liliwafanya waibuke na pointi zote tatu.

Hata kama Barca watashinda michezo yao miwili mkononi, Madrid watakuwa wanaongoza kwa pointi tisa kileleni, A... letico Madrid na Real ... tis pekee ndio wanawe... kuwaletea usumbufu.

Na Ancelotti ana... ambua hilo kuwa Madr... wako karibu kubeba taj...

Aliiambia LaLiga T... "Hapana, haijaisha, lak... iko karibu sana.

"Kila mtu anasub... kushindwa kwa Real M... drid, lakini bado tupo ... nguvu kubwa."

Madrid wameku... wakitoka nyuma na k... pata ushindi katika mi... ya hivi karibuni, hasw... katika Ligi ya Mabingw... Ulaya dhidi ya Paris Sai... Germain na Chelsea.

,243,460

# MSHINDI BET BONANZA AELEZA ATAKAVYOTUMIA MILIONI 15/-

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuibuka mshindi wa droo ya mwisho na kubwa ya Bet Bonanza ya Sportpesa, George Jafari Kimaro, amesema kiasi cha Sh. milioni 15.8 alichoshinda atakitumia kuboresha biashara yake ya mitumba, kununua bodaboda (pikipiki) mbili pamoja na kuisaidia familia yake.

George ambaye jana aliibuka katika ofisi za SportPesa, akielezea furaha yake ya ushindi na mambo mengine, alisema yeye ni fundi ujenzi msaidizi, lakini hiyo haimzuii kununua bodaboda na pia kuongeza mtaji kwenye biashara yake ya mitumba na nyingine kwa maendeleo ya familia yake.

Aidha, George amewashauri Watanzania na wachezaji wenzake waiamini SportPesa kwani ni ya uhakika na hakuna longolongo katika malipo.

Kuhusu historia yake ya kubashiri na SportPesa, George alisema alianza kucheza mwanzoni mwa mwaka jana, lakini alikuwa akiifahamu tangu mwaka 2018, wakati huo akiwa shule na vijana wenzake walikuwa wanacheza, ila kwa kipindi hicho hakujishughulisha nayo.

"Nilipoanza kubashiri mwanzoni nilikuwa natumia simu ya 'tochi', lakini baadaye nikabaini ninakuwa na uwanja mdogo wa kuchagua, hivyo ililazimu kutafuta simu janja ambayo ndio ninayotumia mpaka leo.

"Unajua Sportpesa wako vizuri kwenye app yao na malipo yao ni fasta ndio vinavyonivutia zaidi. Mimi nacheza zaidi 'multibet' na nimewahi kushinda kama mara nne mpaka tano kabla ya ushindi huu. Nakumbuka kiwango cha juu mimi kushinda ilikuwa laki sita, hiyo ilikuwa mwezi wa kumi," alisema.




Mshindi wa Promosheni ya SportPesa Bet Bonanza, George Kimaro kutoka Morogoro, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. 15,888,000 baada ya kushinda kwenye hitimisho la kampeni hiyo. **PICHA: SPORTPESA**

# *Kitayosce yatamba kupanda Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kitayosce imesema imejiandaa kikamilifu kufanya vema kwenye michezo iliyobaki ya Ligi ya Championship ili kutimiza azma yao ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Mkurugenzi wa klabu hiyo, Yusuph Kitumbo, amesema wamebakisha mechi kadhaa, ikiwamo dhidi ya vinara wa ligi hiyo, DTB ambayo inaongoza ligi hiyo kwa muda mrefu, lakini wao wamejiandaa kikamilifu kwa ajili ya kuufanya Mkoa wa Tabora kuwa na timu ya Ligi Kuu msimu ujao.

"Tuko vizuri, tunajiandaa na mechi zilizosalia, mechi zetu ni ngumu, lakini hata wenzetu waliotutangulia zao zilizobaki ni ngumu pia. Mfano ni kwamba hao DTB ambao wanasema eti mechi zetu zilizobaki ni ngumu na wao wanakuja huku Tabora, tunawasubiri kwa hamu, lengo letu msimu ujao ni kucheza Ligi Kuu," alisema Kitumbo.

Aliwashukuru mashabiki wa Tabora kwa kujitokeza kwa wingi wakati timu hiyo inacheza, na kudai kuwa umati unaojitokeza, unazidi hata wale wanaojitokeza kwenye baadhi ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kitayosce inakamata nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi ya Championship ikiwa na pointi 53, ambazo ni sawa na Ihefu inayoshika nafasi ya pili, lakini zikitofautiana mabao ya kufunga na kufungwa. DTB, ndiyo inayoongoza ikiwa na pointi 56, timu zote zikicheza mechi 25, zikibakiza mechi tano.

Timu mbili za juu zitapanda daraja moja kwa moja, huku mbili zilizobaki ya tatu na ya nne zikielekea kucheza mechi za mchujo na timu mbili za Ligi Kuu zitakazomaliza nafasi ya 13 na 14, ili kupata timu mbili za kucheza Ligi Kuu msimu ujao.


## JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/04/22 | 17:00 | Leicester vs Aston Villa | 2.63 | 3.28 | 2.53 |
| 02. 23/04/22 | 17:00 | Hull City vs Reading | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 03. 23/04/22 | 17:00 | Birmingham vs Millwall | 2.78 | 3.08 | 2.53 |
| 04. 23/04/22 | 17:15 | Fuenlabrada vs Ponferradina | 2.57 | 3.16 | 2.67 |
| 05. 23/04/22 | 20:30 | Adana Demirspor vs Trabzonspor | 2.40 | 3.39 | 2.74 |
| 06. 23/04/22 | 21:00 | Waalwick vs PEC Zwolle | 2.46 | 3.07 | 2.87 |
| 07. 23/04/22 | 21:30 | St. Pauli vs SV Darmstadt | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 08. 24/04/22 | 16:00 | Burnley vs Wolverhampton | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 09. 24/04/22 | 16:00 | Bologna vs Udinese | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 10. 24/04/22 | 16:00 | Metz vs Brest | 2.98 | 3.22 | 2.33 |
| 11. 24/04/22 | 17:15 | UD Ibiza Eivissa vs Las Palmas UD | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 12. 24/04/22 | 18:30 | Hertha BSC vs Stuttgart | 2.73 | 3.22 | 2.48 |
| 13. 24/04/22 | 21:45 | Lazio vs AC Milan | 2.78 | 3.27 | 2.41 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 19/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1222 | Sydney FC vs Hoang Anh Gia Lai | 1.51 | 3.84 | 5.65 |
| 14:00 | 2235 | Vissel Kobe vs Kitchee | 1.44 | 4.26 | 5.81 |
| 14:35 | 3259 | Minerva FC vs Gokulam Kerala FC | 2.83 | 3.17 | 2.32 |
| 15:00 | 2506 | Adama City FC vs Hadiya Hosahina FC | 2.49 | 2.68 | 3.07 |
| 17:00 | 3043 | Yokohama F Marinos vs Jeonbuk Hyundai | 2.25 | 3.26 | 2.87 |
| 17:35 | 1722 | Real Kashmir vs Tiddim Road Athlectic Club | 2.14 | 3.26 | 3.07 |
| 18:00 | 3690 | Fasil Kenema vs Addis Ababa City FC | 1.64 | 3.51 | 4.88 |
| 18:00 | 5050 | Bursaspor vs Genclerbirligi | 1.92 | 3.31 | 3.60 |
| 19:00 | 1890 | Skeid Fotball vs Brann | 4.68 | 4.00 | 1.57 |
| 19:00 | 2602 | Mjondalen vs Stjordals-Blink | 1.68 | 3.70 | 4.29 |
| 19:00 | 3429 | Sandnes Ulf vs Kongsvinger IL | 1.91 | 3.50 | 3.45 |
| 19:00 | 4499 | Sogndal vs Bryne | 1.71 | 3.55 | 4.28 |
| 19:00 | 5019 | Aasane Fotball vs Stabaek | 2.82 | 3.41 | 2.21 |
| 19:00 | 5906 | Kfum Oslo vs Raufoss | 1.96 | 3.51 | 3.27 |
| 19:00 | 5935 | Ranheim vs Grorud IL | 1.82 | 3.69 | 3.59 |
| 20:00 | 1366 | Mallorca vs Alaves | 2.16 | 3.19 | 3.39 |
| 20:00 | 2282 | Arsenal Sarandi vs Barracas Central | 1.69 | 3.45 | 4.57 |
| 20:00 | 3745 | Voluntari vs Argesul Pitesti | 2.16 | 2.96 | 3.35 |
| 20:00 | 4990 | Trelleborgs FF vs Ostersunds | 1.98 | 3.44 | 3.79 |
| 20:00 | 5840 | Randers vs Silkeborg | 2.68 | 3.43 | 2.43 |
| 20:15 | 1985 | Wihdat Amman vs Al Sadd SC | 10.72 | 6.04 | 1.19 |
| 20:15 | 5152 | Al Rayyan SC vs Al Sharjah SC | 3.21 | 3.35 | 2.04 |
| 20:45 | 2543 | Slovan Bratislava vs AS Trencin | 1.28 | 5.24 | 7.77 |
| 21:00 | 3193 | Niort vs Bastia | 2.63 | 2.78 | 2.93 |
| 21:00 | 4706 | Amiens vs Le Havre | 2.15 | 3.12 | 3.41 |
| 21:00 | 5937 | Guingamp vs PAU FC | 1.93 | 3.27 | 3.92 |
| 21:45 | 1777 | Cambridge Utd vs Charlton | 2.97 | 3.31 | 2.27 |
| 21:45 | 2634 | Hamburger SV vs SC Freiburg | 3.47 | 3.47 | 2.06 |
| 21:45 | 2762 | Fulham vs Preston | 1.41 | 4.38 | 6.96 |
| 21:45 | 2801 | Glentoran Belfast vs Larne | 2.40 | 3.22 | 2.68 |
| 21:45 | 2888 | Sheffield Wed vs Crewe | 1.17 | 6.37 | 13.94 |
| 21:45 | 2925 | Portadown FC vs Dungannon Swifts | 2.68 | 3.56 | 2.24 |
| 21:45 | 3132 | Ballymena Utd vs Warrenpoint | 1.27 | 5.28 | 8.02 |
| 21:45 | 3496 | Burton vs Rotherham | 4.37 | 3.63 | 1.74 |
| 21:45 | 3590 | Oxford Utd vs MK Dons | 2.31 | 3.27 | 2.93 |
| 21:45 | 4055 | Coleraine FC vs Cliftonville Belfast | 3.06 | 3.06 | 2.24 |
| 21:45 | 5281 | Ipswich vs Wigan | 2.52 | 3.17 | 2.72 |
| 21:45 | 5480 | Carrick Rangers vs Glenavon | 2.97 | 3.55 | 2.07 |
| 21:45 | 5507 | Queen of South vs Inverness | 3.64 | 3.45 | 1.92 |
| 21:45 | 5825 | Crusaders Belfast vs Linfield Belfast | 2.58 | 3.22 | 2.49 |
| 22:00 | 2450 | Betis vs Elche | 1.54 | 4.11 | 5.61 |
| 22:00 | 3771 | Shabab AL Khaleel vs Shabab Alsamu | 1.35 | 4.58 | 7.22 |
| 22:00 | 4644 | Inter vs AC Milan | 1.99 | 3.38 | 3.63 |
| 22:00 | 5501 | Liverpool vs Manchester Utd | 1.39 | 4.85 | 6.54 |
| 22:30 | 2142 | Union Santa Fe vs San Lorenzo | 2.13 | 2.97 | 3.41 |
| 22:30 | 2196 | Villarreal vs Valencia | 1.51 | 4.21 | 5.82 |
| 22:30 | 4775 | El Ittihad Alexandria vs Zamalek | 4.98 | 3.14 | 1.80 |
| 22:30 | 5009 | Talaea El Gaish vs Ceramica Cleopatra | 2.68 | 2.68 | 3.03 |
| 23:15 | 1969 | Al Faisaly (KSA) vs Nasaf Qarshi | 2.44 | 2.83 | 2.97 |
| 23:15 | 4759 | FK Istiklol vs Al Hilal Riyadh | 19.36 | 7.94 | 1.08 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Aprili 19, 2022

Nipashe





Hakimi amtaka Mbappe abaki PSG UKURASA 22

HUNIWEZI...




Winga wa Simba, Peter Banda, akipata upinzani mkali kutoka kwa beki wa Orlando Pirates ya Afrika Kusini, Happy Jele, wakati akimiliki mpira kwenye mechi iliyopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na wenyeji kushinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA**

## Aucho, Fei Toto wamtuliza Nabi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI akiendelea kuiandaa timu yake kuelekea mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Namungo FC, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameelezea kufurahishwa na kurejea kikosini kwa 'majembe' yake tegemeo yaliyokuwa chumba cha majeruhi.

Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 51, Jumamosi wiki hii itaikaribisha Namungo FC kwenye mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa. Akizungumza na mwandishi wetu kuelekea mchezo huo, Nabi alisema kikosi chake sasa kimekamilika na atakuwa na wigo mpana wa kufanya uchaguzi baada ya nyota waliokuwa majeruhi kurejea.

Nabi alisema Khalid Aucho, Feisal Salim 'Fei Toto' tayari wamerejea kikosini na kuanza mazoezi na wenzao na wanaweza kucheza dhidi ya Namungo FC Jumamosi.

Alisema Saido Ntibazonkiza na Fiston Mayele ambao hawakuwa katika ubora wao mechi iliyopita dhidi ya Geita Gold FC sasa wako kamili na anatarajia kuona wakiisaidia Yanga kutoa ushindani mkubwa dhidi ya Namungo.

Yanga itaivaa Namungo ikiwa na kumbukumbu ya kunusurika kichapo katika mechi ya raundi ya kwanza iliyopigwa Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, baada ya kusawazisha kwa penalti dakika za mwisho wakati zikitoka sare ya bao 1-1.

# SIMBA: NI NGUMU KWA ORLANDO PIRATES SAUZI

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

### ●●● Pablo asema ataisuka beki kulinda ushindi, uongozi kujifungia kupanga mikakati, wachezaji kambini...

LICHA ya ushindi wa bao 1-0 walioupata dhidi ya Orlando Pirates katika mechi ya robo fainali ya kwanza iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Klabu ya Simba imekiri itakuwa ni mechi ngumu kwao kuweza kufurukuta mbele ya miamba hiyo ya Afrika Kusini ikiwa uwanja wao wa nyumbani Jumapili wiki hii, lakini watajipanga kuhakikisha wanalinda walichokipata.

**Katika mechi hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba ilipata bao hilo pekee dakika ya 67 kwa mkwaju wa penalti kupitia kwa Shomari Kapombe baada ya Bernard Morrison kuangushwa ndani ya eneo la hatari, hivyo ili kufuzu nusu fainali sasa inapaswa kupata ushindi wowote ama sare yoyote.**

Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, ameliambia Nipashe kuwa anafurahia matokeo hayo, lakini bado ana kazi kubwa ya kuimarisha mabeki wake kuhakikisha wanalinda ushindi wao katika mchezo wa marudiano nchini Afrika Kusini.

Pablo alisema ushindi huo umewapa faida kwenye mchezo wa marudiano ugenini Jumapili wiki hii, na kwamba wanatarajia kupata upinzani mkubwa kutoka kwa Orlando Pirates, lakini watajipanga kuhakikisha wanaenda kufanya vizuri.

Alisema mabeki wanatakiwa kuwa imara kwa sababu ushindi waliopata nyumbani uko katika karatasi na vijana wake kutakiwa kubadilika hasa wanapokwenda kucheza ugenini.

"Lazima tubadilike, tunahitaji kwenda kuonyesha ushindani katika mchezo wa ugenini kuhakikisha tunaenda kuzuia na kutafuta bao la mapema katika mchezo huo wa marudiano.

"Hatukuwa na matokeo mazuri kwenye mechi za ugenini katika hatua ya makundi, hivyo tunapaswa kujipanga na kuwa imara katika safu ya ulinzi hasa kutokana na ubora wa wapinzani," alisema na aliongeza:

"Michuano ya Afrika mara nyingi timu zinafanya vizuri nyumbani kama tulivyofanya, tutajipanga kuelekea mchezo wa marudiano ugenini kwa kuwa tunahitaji kufuzu nusu fainali," alisema Pablo.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', naye amekiri kuwa ni kazi ngumu kuitoa Orlando Pirates kwenye hatua hii ya robo fainali, hivyo kazi kubwa ya ziada inabidi ifanyike kwao kama viongozi, benchi la ufundi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwenye mechi ya marudiano. Akizungumza baada ya mchezo huo wa juzi, Try Again alisema ushindi wa bao 1-0 ni faida kwa Simba na muhimu, lakini wamepata ushindi mwembamba, hivyo inabidi kufanya kazi ya kuanza kuitoa timu hiyo kwao.

"Ni ngumu kushinda mabao mengi, fuatilia timu zote zilizocheza kwenye hatua ya Ligi ya Mabingwa na Shirikisho, hakuna timu iliyoshinda mabao mengi, ushindi ni ushindi ingawa ni mwembamba, kwa sasa tunatakiwa kufanya kazi ya ziada ili kuitoa. Hii sasa ni mipango ya mwalimu na sisi viongozi kuangalia ni jinsi gani tunaweza kwenda kupata sare ugenini au kushinda, kikubwa ni kulinda ushindi wetu.

"Siwezi kusema lolote kuelekea mechi ya marudiano kwanza mpaka viongozi tukae na mwalimu, menejimenti na wadau kuangalia ni namna gani tutafanya kwa ajili ya mechi hiyo. Orlando ni timu nzuri na ina nidhamu, ilituheshimu kwenye mechi hii, tukapata penalti tukaitumia. Simba ni timu kubwa, kwenye hili tunaweza kupita na kusonga mbele kwenye michuano hii," alisema.

Baada ya mechi hiyo wachezaji wa Simba walipewa mapumziko ya siku moja na leo Jumanne watarejea kambini kwa ajili ya maandalizi ya mchezo huo wa marudiano.

Kwa uapnde wa Kocha wa Orlando Pirates, Mandla Ncikazi aliwapongeza Simba kwa ushindi waliupata na kucheza mpira wa ushindani mkubwa katika mchezo huo, lakini akalalamikia penalti haikuwa halali na wao kunyimwa penalti pamoja na mapokezi mabaya waliyoyapata.

"Simba hahitaji msaada wa waamuzi, timu nzuri ina wachezaji wazuri akiwamo Pape Sakho, Shomari Kapombe, Bernard Morrison, Mohammed Hussein, Taddeo Lwanga na Chris Mugalu,"alisema Ncikazi huku akimtupia mwamuzi wa mchezo huo, Haythem Guirat kutoka Tunisia kwa kuwapa Simba penalti na wao kunyimwa baada mchezaji wao kuangushwa ndani ya 18.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >